KUCHUNGUZA UHALISIAJABU KATIKA RIWAYA YA MZIMU WA WATU WA KALE

RAHMA MOHAMED SAID

TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M. A KIWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2019

ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo: **Kuchunguza Uhalisiajabu katika Riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale***, na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Dr. Mohamed Omary

(Msimamizi)

Tarehe .....

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kuzalisha au kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeleo.

IKIRARI

Mimi, **Rahma Mohammed Said**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa wala haitawasilishwa, katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyengine yoyote.

Saini ……

Tarehe……..

SHUKRANI

Kwanza kabisa kabla sijasema neno lolote, napenda nitoe shukrani zangu zisizo na ukomo kwa Mwenyeezi Mungu kwa sababu yeye ndiye Mkuu na anayepaswa kushukuriwa kwa hatua yoyote ya maisha ya mwanadamu. Ninamshukuru kwa kunijaalia afya njema, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nasema kwa unyenyekevu, Alhamdulillah.

Pili, nawashukuru sana wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunifunza kuhusu mambo ya Dunia na Akhera. Vile vile, shukurani za pekee ni kwa mume wangu kipenzi Bw. Rashid Salim Said kutokana na uvumilivu wake, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa.

Tatu, napenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangu Dr. Mohamed Omary Maguo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno linalofaa kutoa shukrani zangu kwake bali namuombea afya njema na maisha marefu ili aendelee kutoa msaada wa kitaaluma kwa wanafunzi wanaohitaji maarifa zaidi ndani na nje ya Tanzania.

Nne, nitakuwa mchache wa fadhila nisipotoa shukrani zangu kwa wale wote walionisaidia kwa hali moja ama nyingine mpaka kazi hii kukamilika, hawa ni wengi sana lakini hapa nitawataja wachache; Bw. Bakar Kombo wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Bw. Ali Mussa Faki, Bw. Sharif Fakih Juma.

Mwisho, nawashukuru wanaidara wote wa idara ya Isimu na Taalimu za Fasihi kwa maoni na miongozo yao hadi leo nimefanikiwa.

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa marehemu wazazi wangu Bw. Mohamed Said Abdalla na Bi. Uvuno Salim Issa na familia yangu yote. Kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi kufikia hapa nilipo. Pia naitabaruku kazi hii kwa muume wangu kipenzi Al-Hajj Rashid Salim Said pamoja na kaka yangu Bw. Sulaiman Mohamed Said kwa kunihamasisha kusoma katika fani hii ya Uzamili. Nawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu (S.W) awasamehe makosa yao na awajaalie wawe miongoni mwa waja wema wa peponi kwa Rehema na mapenzi yake Allah (S.W) Amin.

IKISIRI

Utafiti huu unahusu kuchunguza uhalisiajabu katika Riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Utafiti huu ulihusisha malengo mahsusi mawili ambayo ni kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* na lengo la pili ni kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Katika kuyabainisha na kuyachambua malengo haya, mtafiti ametumia mbinu ya usomaji makini pamoja na upitiaji wa nyaraka maktabani. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya madhumuni maalumu. Aidha, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Utafiti huu uliongozwa na Nadhariaya Uhalisiajabu kwa lengo mahsusi la kwanza na suali la kwanza. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imetumika kwa lengo mahsusi la pili na suali la pili katika muktadha wa Uchambuzi wa Matini za Kifasihi. Utafiti umegundua kuwariwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imetumia vipengele vya uhalisiajabu ambavyo ni wahusika wa kihalisiajabu, mandhari ya uhalisiajabu, uzungumzi nafsi, matukio ya kihalisiajabu, usimulizi wa kihalisiajabu na umahuluti wa kitanzu, kitamaduni na mwingilianomatini. Adha, utafiti umegundua kuwa vipengele hivyo vya uhalisiajabu katika riwaya teule vimeibua dhamira za imani za jadi, uongozi mbaya, ukoloni, utabaka, mauaji, umuhimu wa kutunza kumbukumbu, upelelezi, uganga wa kienyeji, unyonyaji na ukandamizaji na nafasi ya mwanamke. Kwa matokeo haya utafiti huu umebaini kwamba riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imesawiriwa kwa mbinu ya uhalisiajabu kwa kiasi kikubwa kama mtindo wa msanii kuibua dhamira alizozikusudia kwa jamii aliyoiandikia.

YALIYOMO

ITHIBATI ii

HAKIMILIKI iii

IKIRARI iv

SHUKRANI v

TABARUKU vi

IKISIRI vii

YALIYOMO viii

VIFUPISHO xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Mada 1

1.3 Tatizo la Utafiti 6

1.3.1 Malengo ya Utafiti 7

1.3.2 Lengo Kuu 7

1.3.3 Malengo Mahsusi 7

1.4 Maswali ya Utafiti 7

1.5 Umuhimu wa Utafiti 7

1.6 Mipaka ya Utafiti 8

1.7 Muundo wa Tasnifu 9

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA 10

2.1 Utangulizi 10

2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali 10
2.2.1 Maana ya Riwaya 10
2.2.2 Dhana ya Dhamira 13
2.2.3 Vipengele vya Uhalisiajabu 14
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi 15
2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Uhalisiajabu 15
2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Kazi za Mwandishi Muhamed Said Abdulla 20
2.4 Pengo la Utafiti 23
2.5 Mkabala wa Kinadharia 23
2.5.1 Nadharia ya Uhalisiajabu 24
2.5.1.1 Waasisi wa Nadharia ya Uhalisiajabu 25
2.5.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu 25
2.6 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 26
2.6.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 28
2.6.2 Upungufu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 30
2.7 Hitimisho 30

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 32

3.1 Utangulizi 32
3.2 Eneo la Utafiti 32
3.3 Kundi Lengwa 32
3.4 Sampuli na Usampulishaji 33
3.4.1 Sampuli Lengwa 33

3.5 Aina za Data 34
3.5.1 Data za Awali 34
3.5.2 Data za Upili 35
3.6 Ukusanyaji wa Data 35
3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 35
3.6.2 Mbinu ya Usomaji Makini 36
3.6.3 Mbinu ya Upitiaji Nyaraka 36
3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data 37
3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo 37
3.8 Hitimisho 37

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA 39
4.1 Utangulizi 39
4.2 Usuli wa Mwandishi: Mohamed Said Abdulla 39
4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale 42
4.4 Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale ... 43
4.4.1 Usawiri wa Wahusika wa Kiuhalisiajabu 43
4.4.2 Mandhari ya Kiuhalisiajabu 49
4.4.2.1 Mandhari ya Kichaka cha Mzimu wa Watu wa Kale 50
4.4.2.2 Mandhari ya Ndani ya Mzimu 52
4.4.2.3 Mandhari ya Sebule 53
4.4.2.4 Mandhari ya Makaburini 54
4.4.3 Uzungumzinafsi 56
4.4.4 Matukio ya Kiuhalisiajabu 59

4.4.5 Usimulizi wa Kiuhalisiajabu 63

4.4.6 Umahuluti wa Kiutamaduni na Kitanzu na Mwingilianomatini 64

4.5 Dhamira Zilizobainishwa kwenye Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya Teule 66

4.5.1 Imani za Jadi 67

4.5.2 Uongozi Mbaya 70

4.5.3 Ukoloni 71

4.5.4 Utabaka 73

4.5.5 Mauaji 75

4.5.6 Umuhimu wa Kutunza Kumbukumbu 76

4.5.7 Upelelezi 77

4.5.8 Uganga 79

4.5.9 Unyonyaji na Ukandamizaji 81

4.5.10 Mfumo wa Kiuchumi 82

4.4.11 Nafasi ya Mwanamke 83

4.5.12 Utamaduni 84

4.6 Hitimisho 87

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 88

5.0 Utangulizi 88

5.1 Muhtasari wa Tasnifu 88

5.2 Matokeo ya Utafiti 90

5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza 91

5.2.2 Lengo Mahususi la Pili 91

5.3 Hitimisho 92

5.4 Mapendekezo 92

5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine 92

5.4.2 Mapendekezo kwa Watunga Sera 92

5.4.3 Mapendekezo kwa Taifa 93

5.4.4 Mapendekezo kwa Jamii 93

MAREJELEO…… 94

VIFUPISHO

Bi.	Bibi
Bw.	Bwana
DC	District Commisioner
Dkt	Daktari
Dr	Doctor
MA	Master of Arts
Mh	Mheshimiwa
Mw	Mwalimu
OUT	Open University of Tanzania
OUP	Oxford University Press
PhD	Doctor of Philosophy
Prof	Profesa
SUZA	State University of Zanzibar
S.W	Subhanahu Wataalah
TAKILUKI	Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
UDSM	University of Dar es Salaam
Uk.	Ukurasa

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii imekusanya vipengele muhimu ambavyo mtafiti amevifafanua katika utafiti huu. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpango wa utafiti.

1.2 Usuli wa Mada

Dhana ya uhalisiajabu imekuwa ikijadiliwa na kufanyiwa utafiti na wataalamu mbalimbali ulimwenguni. Waliowahi kufanya utafiti wa aina hiyo ni pamoja na Roh (1925), aliyetumia neno uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kueleza aina fulani maalumu ya kudhihirisha usiri ulioko kwenye maisha ya kila siku bila kuupigia maswali yoyote uhalisia huo. Katika kazi za fasihi uhalisiajabu huhusishwa na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia.

Naye Mbatiah (2001)anafafanua kuwa istilahi ya uhalisiajabu inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo, mitindo ya uhalisiajabu inaelezwa kwa njia ya moja kwa moja kama kwamba ni mambo ya kawaida. Anaendelea kusema kuwa wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa, ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokana na maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Kwa maoni ya Mbatiah ni kwamba uhalisiaajabu huhusishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka Bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia.

Wamitila (2004) ana mawazo yanayofanana na nayale ya Mbatiah (2001) kuhusu usuli wa dhana ya uhalisiajabu ambapo anaeleza kuwa dhana ya uhalisiajabu

huhusishwa na Wamarekani wa Kusini au hata nchi zinazoitwa ulimwengu wa tatu. Anaendelea kueleza kuwa sifa yake kuu ni kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu (kichawi) kwa namna ya moja kwa moja, kwa maana inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika.

Vile vile, katika kulieleza suala la uhalisiaajabu Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa uhalisiajabu ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyoelezwa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirirni. Sifa hizo ni kama zile zilizoelezwa na Cooper (1998)ambapo matukio ya kushangaza na kuogofya, huwasilishwa kama kwamba ni hali za kawaida tu.

Alexander (1999)anasema kwambauhalisiajabu ni kielelezo cha nadharia ya usasaleo jinsi inavyotulazimu kufikiria upya juu ya riwaya za kimapokeo kuhusu riwaya za uhalisia za karne ya kumi na nane na tisa. Mtaalamu huyu anaihusisha dhana ya uhalisiajabu na utanzu wa riwaya tu ambapo kwa kweli uhalisiajabu hujitokeza hata katika tanzu nyengine za fasihi kama vile ushairi na tamthiliya.

Tunapozungumzia muasisi wa nadharia ya Uhalisiajabu wataalamu wamekuwa na mitazamo tafauti. Warnes (2002)anadai kwamba matumizi ya awali kabisa ya istilahi ya uhalisiajabu yanapatikana katika maandishi ya mshairi Friedrich Freiherr von Hardenberg maarufu kama Novalis (1772-1801).

Mawazo mengine kuhusu muasisi wa nadharia ya uhalisiajabu ni yale ya Zamora na Faris (1995) ambao wanaeleza kwamba nadharia ya Uhalisiajabu iliasisiwa mwaka

wa 1925 na Mjerumani Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Wanaendelea kusema kwamba Franz ndiye alietumia istilahi ya uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa ili kuelekeza na kuonyesha aina fulani ya uajabu au mazingaombwe yaliyomo kwenye uhalisi uliozoeleka na unaotokana na ujaribati.

Aidha, Zamora na Faris (2005)wanadai kuwa uhalisiaajabu unaafiki kutalii na kukaidi mipaka ya kiontolojia, kisiasa, kijiografia au kiutanzu. Hivyo uhalisiajabu unapaswa kueleweka kama mkabala unaowakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu na kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha. Pamoja na kuwa ni mkabala wa kifasihi unaonasibishwa zaidi na waandishi wa Amerika Kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za janibu mbalimbali zikizungumziana kwa dayalojia hii.

Naye Abrams (1999)anasema kuwa dhana ya uhalisiajabu ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, ilitumika kufasili kazi bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina pamoja na kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia na Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia na John Fowles wa Uingereza. Aidha, waandishi hawa wanaendeleza uhalisia uliosanwa kwa njia maalumu katika sheria inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto na kwa kutumia mambo yaliyotokana na yanayobadilikabadilika daima.

Katika kuchangia mjadala huu Green (2009)anasisitiza kuwa mitindo na misingi ya Uhalisiajabu katika fasihi, kimatendo ilikuwa ya awali zaidi hasa katika kaida za

Kiramsia (*RomanticisAidham*) ambapo masimulizi yaliwekwa sambamba na matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida.

Katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili utafiti huu unaiona dhana ya Uhalisiajabu kuwa ni kongwe na ilianza tangu watumiaji wa fasihi walipoanza kutumia fasihi simulizi hasa ile inayohusu ushairi simulizi na hadithi simulizi. Mawazo haya yanaungana na yale ya Wamitila (2013) na Senkoro (2011) ambao wanaona kwamba uhalisiajabu ni mtindo unaohusishwa na fasihi simulizi na wanatolea mfano riwaya za Shaaban Robert kama vile*Kusadikika, Adili na Nduguze na Kufikirika* ndizo zilizochota vipengele vya uhalisiajabu kwa vile zimechota vipengele vya fasihi simulizi. Kasoro kubwa ya mawazo ya Wamitila na Senkoro ni kwamba hawakuzibainisha kazi za waandishi wengine kama zile za Mohamed Said Abdulla ambazo pia zina vipengele vya uhalisiajabu.

Miaka ya hivi karibuni, katika fasihi ya Kiswahili kumejitokeza kazi ambazo zimeandikwa kwa mkabala wa Uhalisiajabu. Khamis (2005)anasema riwaya za *Nagona* na *Mzingile* za mwandishi Kezilahabi, *Babu Alipofufuka* ya Said Ahmed Mohamed na *Bina-Adamu* ya Wamitila ni miongoni mwa riwaya za kisasa ambazo zimesheheni mitindo ya uhalisiajabu.

Waliaula (2010)anaeleza kwamba nadharia ya uhalisiajabu ni nadharia ambayo ilinasibishwa na Amerika ya Kusini sasa imepenya mpaka Afrika ya Mashariki ambapo inatumiwa na waandishi mbalimbali katika kukusanya kazi zao za fasihi. Miongoni mwao ni Ngugi wa Thiong’o katika riwaya yake ya *Murogi wa Kagogo*(2004). Aidha waandishi wengine ni Waliaula (2010) alichunguza uhalisia na

uhalisia mazingaombwe: mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum,* aligundua kuwa uhalisia mazingaombwe unafaulu pale ambapo mtindo wa kiuhalisia unashindwa hasa kuhusiana na itikio la wasomaji.

Senkoro (2007)amewataja waandishi mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili wanaoutumia au waliotumia nadharia hii kama vile James Mbotela wa riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934), Shaaban Robert katika riwaya za *Kusadikika* (1951), *Kufikirika* (1969), *Siku ya Watenzi Wote* (1968), *Utubora Mkulima* (1968) na *Adili na Nduguze* (1972). Pia waandishi wengine aliowataja ni pamoja na Muhammed Said Abdulla, E. Mbogo, W. E. Mkufya, E. Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed.

Ibrahim (2016)anaeleza kuwa miongoni mwa waandishi walioathiriwa na nadharia ya uhalisiajabu ni Said Ahmed Mohamed katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) na hadithi fupi ambazo ni *Sadiki Ukipenda* na *hadithi nyengine* (2002) na *Arusi ya Buldoza* na *hadithi nyengine* (2005).

Katika fasihi ya Kiswahili zipo kazi kadhaa ambazo zimefanyiwa uchunguzi kwa kutumia mkabala wa Uhalisiajabu. Miongoni mwa kazi hizo ni ile yaMagaju (2004) alichunguza uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* na *Bin-Adamu* na aligundua kuwa riwaya hizi zimetumia uhalisiajabu kimakusudi kama mkakati unaowawezesha kujadili maswala na kumulika matatizo ya kiuchumi na ya kijamii yanayowakabili Waafrika kutokana na utawala finyu wa viongozi wao na kuupiga vita utandawazi na ubepari wa kimataifa.

Sababu ya mtafiti wa kazi hii kufanya utafiti huu ni kwamba ingawa kuna tafiti kadhaa zimewahi kufanyika kwa lengo la kuchunguza vipengele vya Uhalisajabu

katika riwaya za Kiswahili, lakini mtafiti wa kazi hiikatika utalii wa kazi mbali mbali alibaini kwamba suala la kuchunguza vipengele vya Uhalisiajabu na namna vinavyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* bado halijaangaziwa. Kwa mantiki hiyo utafiti huu uliona ipo haja ya kufanya utafiti huu ili kulithibitisha suala hilo kwa misingi ya sayansi.

1.3 Tatizo la Utafiti

Suala la Uhalisiajabu si geni katika fasihi za ulimwengu ikiwemo fasihi ya Kiswahili. Tafiti kadhaa zimewahi kufanyika ili kuchunguza Uhalisiajabu. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na ule wa Ibrahim (2010), Waliaula (2010), Mutiso (2012), Wanjiru (2013), Wamitila (2013) na Kagendo (2014). Mathalani, Waliaula (2010)alichunguza *Uhalisi na Uhalisia Mazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum*, Wanjiru (2013)alichunguza *Uhalisiajabu katika Riwaya Mpya: Babu alipofufuka na Watu wa Gehenna.* Kagendo (2014)alichunguza *Uhalisia katika riwaya ya Babu Alipofufuka na Bin-Adamu.*Katikautafiti huo aligundua kuwa uhalisiajabu umejitokeza katika vipengele vya wahusika na mandhari.

Mtafiti ametalii machapisho kadhaa lakini hakuona utafiti ambao ulifanyika kwa lengo la kuchunguza vipengele vya Uhalisiajabu na namna vinavyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ya Mohamed Said Abdulla. Hivyo basi, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kutaka kubaini namna riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* inavyotumia vipengele vya uhalisiajabu na jinsi vipengele hivyo vilivyotumiwa na msanii kuibua dhamira ili kuziba mwanya ulioachwa wazi na watafiti wengine.

1.3.1 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi mawili kama inavyojibainisha katika sehemu zifuatazo.

1.3.2 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

1.3.3 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya utafiti huu ni mawili ambayo ni:

i. Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

ii. Kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali mawili ya utafiti yafuatayo:

i. Ni vipengele gani vya uhalisiajabu vilivyojitokezakatika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

ii. Ni dhamira zipi zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaonekana kuwa na msaada mkubwa sana katika nyanjaza kijamii, kitaaluma na hata kinadharia. Msaada wake katika vipengele hivyo umeelezwa na mtafiti wa kazi hii kama ifuatavyo:

Moja: Utafiti huu utaweza kuisaidia jamii kuyaangalia mambo yasiyo ya kawaida ambayo yana uhusiano nayo kama vile uchawi, mashetani, ushirikina na ndoto. Mambo hayo ni muhimu kutambuliwa na jamii kwa kuwa yameshikamana moja kwa moja na mila, tamaduni na jadi za jamii za Waswahili wa ukanda wote wa pwani ya Afrika Mashariki napengine hata Waafrika wa maeneo mengine.

Pili: Utafiti huu umekuwa na faida kubwa kwa watafiti kwa vile wataongeza maarifa ya utumiaji wa nadharia ya uhalisiajabu katika kazi ya fasihi kama riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi.

Tatu: Utafiti huu pia unaweza kutumikakama marejeleo kwa wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo vikuu, walimu na watafiti tarajiwa.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita kuchunguza vipengele vya Uhalisiajabu namna vipengele hivyo vinavyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ya Mohamed Said Abdulla. Mwandishi huyu ametunga riwaya nyingi zikiwemo *Mzimu wa Watu wa Kale* (1966), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani Kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974), *Mke Mmoja Waume Watatu* (1975), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) na *Kosa la Bwana Msa* (1984). Kwa vile Mohamed Said Abdulla ametunga kazi nyingi za fasihi hivyo isingekuwa rahisi kuzitafiti kazi zake zote. Kwa sababu hiyo mtafiti aliteua riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambayo aliamini itaweza kujibu maswali ya utafiti huu. Kuchaguliwa kwa riwaya hii kunatokana na mtafiti kuamini kwamba utafiti huu utaweza kuyajibu au kuyafikia malengo ya utafiti pia kujibu maswali ya utafiti huu.

1.7 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu umegawanywa katika sura tano (5) zifuatazo: -

Sura ya kwanzaKatika sura hii mtafiti amewasilisha vipengele muhimu vya utangulizi navyo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu.

Katika sura ya pili mtafiti ameshughulikia mambo ya msingi yafuatayo: utangulizi wa sura, ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi zinazohusiana na mada ya utafiti pamoja na mapitio ya kazi za mwandishi Mohammed Said Abdulla. Aidha katika sura hii mtafiti amewasilisha nadharia ya Uhalisiajabu na Mwitiko wa Msomaji ambazo zilitumika kuchambua data za utafiti. Kwa kumalizia sura hii mtafiti ameweka hitimisho.

Sura ya tatu mtafiti ameshughulikia vipengele muhimu ambavyo ni: Utangulizi, mbinu za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data, mbinu za kukusanya data, uchambuzi wa data, usahihi wa data za utafiti, maadili ya utafiti na hitimisho.Sura ya nne mtafiti amewasilisha usuli wa mwandishi, muhtasari wa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Pia, katika sura hii mtafiti ameshughulikia uchambuzi wa data za utafiti na hitimisho. Katika suraya tano **v**ipengele ambavyo vimejadiliwa katika sehemu hii ni muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni urejeleaji wa kazi mbalimbali zilizofanywa huko nyuma kwa lengo la kupata maarifa yaliyotokana na maandishi ya watafiti mbalimbali ambao hutoa taarifa kuhusu mada, nadharia na mbinu za utafiti zilizotumika. Wataalamu wa utafiti wanatilia nguvu kwa kusema kuwa mapitio ya kazi tangulizi ni mpangilio maalumu na ufafanuzi wa uchambuzi wa maandishi kuhusu habari inayohusiana na suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi ni lazima yaonyeshe uhusiano ya wazi kati yake na maandishi ya mada husika. (Enon 1998)anasema kuwa mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina unaofanywa kwa nia ya kuchunguza mbinu, nadharia, kutafuta taaluma zinazohusiana na mada zinazofanyiwa utafiti. Maarifa yanayopatikana hutumika katika kuongoza ukusanyaji na uchambuaji wa data kuhusiana na mada inayotafitiwa (Mwakamele, 2013). Kwa ujumla mtafiti amepitia kazi mbalimbali za tafiti tangulizi ambazo zimemsaidia kwa kiwango kikubwa katika kuyafikia malengo ya mada yake husika.

2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali

2.2.1 Maana ya Riwaya

Wataalamu mbalimbali wameifasili dhana ya riwaya kwa mitazamo tofauti. Muhando na Balisidya (1976)wanasema kuwa riwaya ni kazi ya kubuni, ni hadithi ambayo hutungwa kufuatana na uwezo wa fanani kuibusha mambo kutokana na mazoea au mazingira yake. Aidha riwaya yaweza kuanzia maneno 35000 hivi na kuendelea.

Kupitia fasili hii mtafiti ameona kwamba bado suala la maana ya riwaya linahitaji kujadiliwa. Hii ni kwa sababu mtafiti haoni ulazima wa riwaya kuwa na idadi maalum ya maneno bali cha kuzingatia zaidi ni kuwa riwaya iwe na vigezo muhimu ambavyo vitafuatana na visa pamoja na matukio yanayoendana na maisha ya jamii inayoandikiwa.

Naye Nkwera (1978)anasema kuwa riwaya ni hadithi iliyo ndefu kuweza kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi. Anaendelea kufafanua kuwa ni hadithi ya kubuniwa iliyojengwa juu ya tukio la kihistoria na kuandikwa kwa mtindo wa ushairi uendao mfululizo kwa kinaganaga katika kuelezea maisha ya mtu au watu na hata taifa. Pia anaeleza kwamba, riwaya inaweza kuwa na mhusika mmoja au hata wawili. Kupitia fasili ya mtaalamu huyu, mtafiti anaunga mkono maelezo hayo kwa vile yamegusia maneno muhimukama vile hadithi ndefu, ya kubuni, yenye mtiririko wa matukio, wahusika na iendane na jamii husika.

Kwa upande wao Ndungo na Mwai (1991)wanaelezea kuwa riwaya ni sanaa ya nathari inayoelezea hadithi kwa mtiririko na kwa njia ya matukio na vituko vinavyojiri katika muamano wa wakati. Mtafitianaungana na maelezo ya wataalamu hawa kwa vile wamehusisha vipengele muhimu ambavyo ni pamoja na sanaa, mtiririko wa matukio na wakati.

Aidha Mulokozi (1996)anasema kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi.

Mtafiti anakubaliana na maelezo ya Mulokozikwa vile amezungumzia vipengele muhimu kama vile kinathari, urefu wa kutosha, wahusika, dhamira, wakati na maisha halisi.

Senkoro (1982)anaeleza kuwa riwaya ni kisa ambacho ni kirefu kiasi cha kutosha chenye zaidi ya tukio moja ndani yake. Anaendelea kusema kuwa ni kisa mchanganyiko ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani wa mambo mbalimbali. Aidha riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kutambwa mahali pengi na kuumbaa vizingiti vingi kama apendavyo mwandishi.

Ama kwa hakika mtafiti anaunga mkono maelezo ya Senkoro (ameshatajwa) kwa sababu maelezo yake yamezingatia mambo muhimu ambavyo ni pamoja na kisa kirefu, chenye zaidi ya tukio moja, kinachochambuliwa na kupimwa kwa kiwango cha uchangamano. Hivyo basi katika utafti huu mtafiti aliona kuwa mawazo haya yalikuwa na maana sana katika kuyafuatilia matukio ambayo hatimaye yamemuwezesha kulifikia lengo la kwanza la utafiti huu.

Naye Mlaga (2017) anaeleza kuwariwaya ni mchangamano wa visa na matukio unaoilazimisha hadithi husika iwe na urefu wa kutosha, ili kukamilisha mtiririko wa visa na matukio yasimuliwayo.Fasiliya Mlaga (ameshatajwa), mtafiti anaiunga mkono kwa sababu imetilia mkazo juu ya mchangamano wa visa na matukio.

Kwa ujumla baada ya kutalii mawazo mbalimbali yanayohusu dhana ya riwaya mtafiti anahitimisha kwa kusema kwamba riwaya ni utanzu wa kinathari ambao unahusu kisa kirefu cha kubuni chenye zaidi ya tukio moja, wahusika wengi wenye

tabia mbalimbali na ambayo huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa undani kwa kuzingatia fani na maudhui yaliomo ndani yake kutokana na kusawiri maisha halisi ya jamii na mazingira yake.

2.2.2 Dhana ya Dhamira

Dhana ya dhamira imezungumzwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na Senkoro (1982)ambaye anasema kuwa dhamira ni jumla ya mambo yanayojadiliwa katika kazi za fasihi. Senkoro (ameshatajwa) anasema kuwa, dhamira za kazi za fasihi hujitokeza kulingana na matukio ya jamii, wakati, mabadiliko ya jamii na historia ya jamii.

Nao Saluhaya na Suleiman (2012)wanaeleza kuwa dhamira ni kiini cha masuala au makusudio yanayozungumziwa na mtunzi wa kazi za fasihi inayohusika. Anaendelea kusema kuwa dhamira ni kusudio au lengo la mtunzi wa kazi za fasihi. Mlaga (2017)anaeleza kuwa dhamira ni wazo linalomshughulisha mwandishi au msanii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mlaga anaona kuwa yale ambayo yanamsukuma msanii kuyaandikia katika jamii yake ndiyo huwa ni dhamira. Hii ni kusema kuwa kazi ya fasihi huweza kujengwa ikiwa na dhamira zaidi ya moja kutegemea malengo ya msanii.

Kwa ujumla mtafiti anaweza kusema kwamba dhamira ni wazo au mawazo yaliyotawala katika kazi ya fasihi katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Aidha, kazi ya fasihi inaweza kuwa na dhamira kuu moja au mbili pamoja na dhamira ndogondogo. Mara nyingi dhamira katika kazi ya fasihi hubainishwa na hadhira na hata wasomaji

wa jamii husika. Katika utafiti huu, kipengele cha dhamira kitatumika kwa sababu ndio msingi wa lengo mahsusi la pili la utafiti huu.

2.2.3 Vipengele vya Uhalisiajabu

Vipengele vya uhalisiajabu katika kazi za fasihi vinaweza kuelezwa kuwa ni yale mambo au matukio yote yanayoibua maajabu katika kazi za fasihi. Matukio hayo huwa yamekiuka uhalisi wa kijamii. Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakijadili na kuvianisha vipengele ambavyo huibua Uhalisiajabu. Kwa mfano, Waliaula (2010) alifafanua vipengele vya uhalisiajabu na kuonesha kwamba Uhalisiajabu hujikita katika vipengele vya usimulizi, wahusika, matukio ya kiuhalisiajabu. Mawazo haya ya Waliaula yalikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kutokana na kwamba mtafiti alivichunguza vipengele vya Uhalisiajabu kama vilivyojadiliwa na Waliaula jambo ambalo lilirahisisha katika ukusanyaji wa data za utafiti huu.

Naye Wamitila (2013) amebainisha vipengele mbalimbali vya Uhalisiajabu vinavyotumiwa na wasanii katika kuumba kazi za kifasihi. Vipengele hivyo ni kama vile uhalisiajabu na mitindo na mbinu za kisimulizi, mgotanisho wa uhalisi na njozi au fantasia, michezo na utatizaji wa dhana ya wakati, mitindo ya udenguzi na uumbuzi, umahuluti wa kitamaduni na kitanzu na mwingilianomatini, usawiri wa wahusika, utambulisho na mwanda wa kiuhusika, ishara na uashiriaji na suala la uchimuzi na uhalisia ajabu na masuala ya Ontolojia. Mawazo haya ya Wamitila ambayo yalilenga kubainisha vipengele vya Uhalisiajabu yalikuwa ni msingi mkuu katika kufikia lengo mahususi la kwanza. Msanii alichunguza kwa makini namna riwaya teule ilivyovitumia vipengele hivyo hatimaye mtafiti alifanikisha kujibu swali la kwanza la utafiti huu.

Aidha, Mturo (2018) ameeleza vipengele vya uhalisiajabu, ambavyo ni matukio ya kiuhalisiajabu, mipaka ya wakati pamoja na mwanda na utambulisho, usimulizi wa kiuhalisiajabu, matumizi ya ishara zisizokubalika kiuhalisia, wahusika wa kiuhalisiajabu na mandhari ya uhalisiajabu. Mawazo haya ya Mturo kama yalivyokuwa ya watangulizi wengine nayo yalimpatia mtafiti uelewa wa kina kuhusu vipengele vinavyohusishwa na dhana ya uhalisiajabu. Kwa hivyo mtafiti aliyachukua mawazo hayo na kumuongoza wakati wa kukusanya data za utafiti huu.

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Uhalisiajabu

Mtafiti alitalii machapisho kadhaa na kugundua kuwa dhana ya uhalisiajabu imewahi kushughulikiwa na waandishi kadhaa. Baadhi yao ambao wamewahi kuishughulikia dhana ya Uhalisiajabu ni pamoja na Magaju (2004), Nyambunga (2005), Olali (2010), Wamitila (2008 na 2013), Waliaula (2010), Osore (2013), Wanjiru (2013) na Ibrahim (2016). Miongoni mwa kazi hizo ni kama ifuatavyo:

Magaju (2004)alitafiti mada isemayo *“Kuchunguza Uhalisiajabu katika Riwaya ya Babu Alipofufuka na Bin-Adamu”*. Katika utafiti wake amegundua kuwa riwaya hizi zimetumia uhalisiajabu kimakusudi kama mkakati unaowawezesha kujadili maswala na kumulika matatizo ya kiuchumi na ya kijamii yanayowakabili Waafrika kutokana na utawala finyu wa viongozi wao na kuupiga vita utandawazi na wa kimataifa. Mbali na hayo Magaju (ameshatajwa) anaeleza kuwa riwaya ya *Babu Alipofufuka* na *Bina-Adam* zimetumia nadharia ya uhalisiajabu katika kufikisha ujumbe kwa wasomaji wake. Aidha ameidhihirisha mihimili ya nadharia hiyo iliyotumika ili kuibua ujumbe ambao ni pamoja na matukio ya kiajabuajabu, uduara wa wakati,

ndoto na uhalisia, uvunjwaji wa mipaka na maadili, visasili na upekee wa mtindo wa riwaya ya kiuhalisiajabu.

Katika utafiti huo Magaju (ameshatajwa) amebainisha dhamira zilizoibuliwa katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Bina-Adamu* kupitia mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu.Ingawautafiti huu ulifanyika katika riwaya tofauti na ya mtafiti aliyoitafiti, utafiti huu umemsaidia mtafiti katika kufikia malengo mahsusi ya utafiti huu kwa vile tafiti hizi zilikuwa na uwiano katika kipengele cha malengo. Pia utafiti ulikuwa ni dira iliyomwoongoza mtafiti katika ukusanyaji data za utafiti huu.

Vile vile, Nyambunga (2005)alifanya utafiti juu ya mada inayoitwa *"Sifa za Kiuhalisiajabu katika Riwaya ya Musa Leo*na *Babu Alipofufuka"*. Mtafiti aliweza kuyaangazia matukio ya uhalisiajabu katika kazi yake kwa kutaja matukio yanayozua uhalisiajabu katika riwaya ya *Musa Leo na Babu Alipofufuka.*

Nyambunga (ameshatajwa) katika utafiti wake amebainisha matukio ya uhalisiajabu ambayo ni miongoni mwa vipengele vya uhalisiaajabu. Ni wazi kuwa kupitia utafiti huu mtafiti alifaidika kwa kupata mwongozo wa kubainisha matukio ya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

Khamis (2007)akimrejelea Hart (2003)aliandika mada iitwayo *"Uchambuzi juu ya riwaya mpya ya Kiswahili kuhusu namna riwaya hiyo inavyosawiri hali halisi ya maisha katika jamii"*. Katika utafiti wake aligundua kuwa riwaya mpya za Kiswahili hutumia vipengele vya kimazingaombwe kusawiri maisha katika uhalisia wake. Miongoni mwa vipengele hivyo ni wahusika wa kiajabuajabu, mandhari tata isiyofahamika kwa wepesi na muundo usiojulikana mwanzo wala mwisho wake.

Hart (ameshatajwa) amebainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya vinavyoibua dhamira katika jamii. Hivyo maelezo hayo yalimsaidia mtafiti katika kubainisha na kuchambua dhamira zinazoibuliwa na nadharia ya uhalisiaajabu kupitia vipengele vyake.

Wamitila (2008) amezungumzia mada yake ya *"Misingi ya Uchanganuzi wa Riwaya"*. Katika mada hiyo alizielezea riwaya ya kihalisiajabu kuwa huwa na sifa zinazokiuka kaida za uhalisi na ambazo zinajulikana na wasomaji. Pia huwa na matukio ambayo ni vigumu kuyaeleza katika uhalisi, ameeleza mifano ya matukio katika riwaya ya *Mzingile* (1991) ambapo mhusika Kakulu namna alivyoongea, kutania watu na kukimbia mara tu baada ya kuzaliwa. Kwa upande wa riwaya ya *Dharau ya Ini* ameeleza namna fuvu lilivyomfukuza mhusika Munene.

Kazi hiyo ilimpatia uelewa wa kina mtafiti kuhusu vipengele vya Uhalisiajabu. Hivyo ni wazi kuwa mtafiti aliweza kukusanya data katika riwaya teule kwa umakini mkubwa huku akiamini kuwa hakuna dosari itayojitokeza. Kwa kufanya hivyo aliweza kubainisha vipengele vya uhalisiajabu vilivyojitokeza katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

Olali (2010)amefanya utafiti juu ya mada isemayo *"Uhalisiajabu katika Riwaya ya Babu Alipofufuka"*. Katika utafiti wake ameelezea sifa za uhalisiajabu. Aidha amefafanua namna uhalisiajabu ulivyojidhihirisha katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kupitia vipengele vya wahusika, mtindo na matukio.

Olali (ameshatajwa) ameangazia sifa na vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. Hivyo ni dhahiri kuwa utafiti huu ulimsaidia mtafiti katika kuibua

uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kupitia vipengele vya wahusika, mtindo na matukio ambavyo vilitumika katika utafiti uliotangulia.

Aidha, Waliaula (2010) alifanya utafiti katika mada inayoeleza *"Kuchunguza uhalisia na uhalisia mazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum"*. Katika utafiti wake aligundua kuwa uhalisia mazingaombwe unafaulu pale ambapo mtindo wa kiuhalisia unashindwa hasa kuhusiana na itikio la wasomaji. Aidha alibainisha vipengele vya uhalisiajabu kama vile mtindo, wahusika, matukio na lugha katika utafiti wake.

Katika dondoo hii ni wazi kuwa Waliaula (ameshatajwa) amebainisha baadhi ya vipengele vya uhalisiajabu. Hivyo mtafiti anaamini kuwa utafiti huo ulimsaidia katika kubainisha na kuchambua vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya yake teule ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

Wanjiru (2013) aliandika mada isemayo *"Kuchunguza uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya mpya: Babu Alipofufuka (Said Ahmed Mohamed) na Watu wa Gehenna (Tom Olali)."* Katika utafiti huo aligundua kuwa uhalisiajabu umejitokeza katika vipengele vya wahusika na mandhari, kwa sababu waandishi hawa wawili wametumia wahusika wa kiajabu pamoja na mandhari yenye matukio mengi ya kiajabu.

Utafiti wa Wanjiru (ameshatajwa) ulikuwa na faida kubwa kwa mtafiti. Hii ni kwa sababu ya kufafanua baadhi ya vipengele vya uhalisiajabu ambavyo ni wahusika na mandhari. Ni ukweli usiopingika kuwa dondoo hii ilimsaidia mtafiti katika

kudhihirisha vipengele vya wahusika na mandhari ambavyo viliibua uhalisiajabu katika utafiti wake.

Osore (2013) alitafiti katika makala yake yenye mada: *"Uhalisia mazingaombwe na uhalisiajabu katika riwaya ya Said Ahmed Mohamed ya Babu Alipofufuka"*. Katika makala hiyo alichambua dhana ya uhalisia mazingaombwe kwa kutumia ushahidi wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* kupitia kipengele cha muhusika na uhusika wake.

Kutokana na utafiti huo wa Osore (ameshatajwa) uliochambua uhalisiajabu kwa kutumia riwaya ya *Babu Alipofufuka*, ni wazi kuwa utafiti huo ulikuwa ni mwongozo na dira kwa mtafiti. Kwa vile aliweza kubainisha na kuchambua uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

Ibrahim (2016) alichambua mada: *"Vipengele vya uhalisiamazingaombwe katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyengine"* Katika utafiti huo, amegundua kuwa uhalisiamazingaombwe umejitokeza katika vipengele vya matukio, mandhari, wahusika na uzungumzi nafsi.

Ni dhahiri kuwa makala hii imejadili vipengele vya uhalisiajabu. Hivyo hali hii imemsaidia na kumpa nguvu mtafiti katika kubainisha uhalisiajabu na vipengele vyake vitakavyojitokeza katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Aidha mtafiti aliweza kutekeleza lengo lake la kwanza na la pili la utafiti wake sambamba na kujibu suali la kwanza na la pili la utafiti wake.

Mtafiti ameeleza wataalamu mbalimbali walioshughulikia uhalisiajabu na matokeo ya tafiti zao. Ambapo tafiti hizo zimekuwa na mchango mkubwa na muhimu wa

kuweza kuufikia utafiti wake. Hivyo aliweza kuuthamini mchango wao ili kufanikisha utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza uhalisiajabu katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale.*

2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Kazi za Mwandishi Muhamed Said Abdulla

Mwandishi Muhamed Said Abdulla ni mwandishi wa riwaya ambaye ameandika vitabu vingi vya riwaya kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale* (1966), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani Kuna Watu* (1973), Siri ya Sifuri (1974), *Mke Mmoja Waume Watatu* (1975), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) na *Kosa la Bwana Msa* (1984). Aidha waandishi mbalimbali wametafiti na kuandika kazi kadhaa kuhusu riwaya zake, miongoni mwa kazi hizo ni kama zifuatazo:

Abdalla (2015)ameandika makala inayosema *"Kosa la Bwana Msa na washauri wa Benki za Kiislamu"*. Katika makala mwandishi anawataka washauri hao wawe na ujuzi wa kile wanachokisema kuwambia watu wengine. Hasa suala hilo likiwa linahusu sharia za Mola Muumba ili kuepuka kufanya makosa kama aliyoyafanya Bwana Msa katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*. Kosa lenyewe lilikuwa kumuoza mke wa mtu mume mwengine na akazaa naye na kurithi mali ya mume huyo alipofariki. Aidha, kwa mume wa mwanamke huyo alidhurika hadi kuwa mwenda wazimu kwa kumkosa mke aliyempenda kwa dhati. Hivyo aliwataka washauri kuwa makini katika ushauri wao na linapotokea kosa kulielezea na kulirekebisha bila kujionea haya kama alivyofanya Bwana Msa katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*. (www.likedin.com)

Makala hii ya Abdalla (ameshatajwa) ilimsaidia mtafiti kumuongoza katika mada yake husika. Kwa vile alikuwa makini katika kubainisha na kuchambua data za uhalisiajabu kupitia vipengele vyake ili kuepuka kufanya makosa. Makosa ambayo yanaweza kuzorotesha utafiti wake.

Mkindi (2016)ameandika makala inayoitwa *"Maudhui katika kazi za fasihi"*. Katika makala hiyo alichambua kipengele cha dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Dhamira alizozigusia ni pamoja na upelelezi, athari za dhuluma, hali ngumu ya maisha, uchoyo, ubahili, dhana patofu na imani za ushirikina, matabaka, umuhimu wa subira, umuhimu wa elimu, umuhimu wa kuthamini lugha ya Kiswahili, kutokata tamaa, ujasiri, suala la dini, nafasi ya vyombo vya dola, umoja na mshikamano, uzalendo, kutokuwajibika, athari za kulipiza kisasi na fitina, mapenzi na ndoa. Aidha mwandishi wa makala hii ametaja baadhi ya riwaya zinazoshabihiana na maudhui ya riwaya hii kama vile *Sumu ya Kifo* (1965) ya mwandishi Katalambula, *Kisima cha Giningi* (1968) na *Duniani Kuna Watu* (1973) zote za mwandishi Mohammed Said Abdulla, *Dimbwi la Damu* (1984) ya mwandishi Ben Mtobwa.

Ni wazi kabisa mwandishi wa makala hii amechambua kipengele cha dhamira katika maudhui ya kazi ya fasihi. Jambo ambalo lililopelekea kutoa mwanga kwa mtafiti wa kazi hii. Hivyo makala hii ilimsaidia mtafiti wa utafiti huu kuibua dhamira zilizojitokeza kupitia vipengele vya uhalisiajabu.

Kisima cha Maarifa (2018) wameandika makala inayohusiana na riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambapo wamechambua dhamira katika riwaya hiyo. Dhamira walizochambua katika makala hiyo ni upelelezi, dhuluma, hali ngumu ya maisha na

umaskini, uchoyo na ubahili, umoja na mshikamano, kutowajibika, ujasiri, uvumilivu na kutokata tamaa, kujitoa muhanga, umuhimu wa kuthamini lugha ya Kiswahili, rushwa, mapenzi, ndoa na nyenyinezo.

Makala hii imechambua dhamira mbali mbali katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Hivyo ni wazi kuwa makala hii ilimsaidia mtafiti kuibua dhamira zinazotokana na uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kupitia baadhi ya mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu.

Koenings (2018), aliandika makala inayosimulia sehemu ya 1 mpaka ya 10 ya riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*. Makala hio imemgusia Bwana Msa na maisha yake ya upelelezi. Aidha maisha ya Amanullah na Sichana baada ya kufukuzwa na bibi yao mlezi bila ya hatia. Katika makala hii zimejitokeza dhamira kama vile hali ngumu ya maisha, upelelezi, umuhimu wa elimu, ukatili, ukosefu wa huduma muhimu, suala la dini, udhalilishaji, nafasi ya vyombo vya dola na mapenzi. Aidha uhalisiajabu umetajwa katika makala hii kupitia ndoto ambazo zinageuka kuwa kweli. Kwa mfano Amanullah alikuwa mara kwa mara anaota kuwa mafanikio yake yako Dar es Salaam, hivyo alifunga safari kuelekea huko. Baada ya muda alitafutwa na polisi ili kurudi Zanzibar kutambuliwa na baba yake aliyomkosa miaka mingi.

Makala hii imeweza kutaja baadhi ya vipengele vya uhalisiajabu ambayo vilimsaidia na kumuongoza mtafiti katika utafiti wake. Kwa vile ilimpa mwanga mtafiti na uwezo wa kuchambua dhamira kupitia vipengele vya uhalisiajabu. Na kuweza kujibu swali lake la pili la utafiti huu.

Kwa hakika, mtafiti amebainisha kazi tangulizi mbalimbali kupitia wataalamu kadhaa waliotafiti katika riwaya za Muhamed Said Abdulla. Mchango wa kazi hizo ulithaminiwa na mtafiti ili kuweza kutekeleza vyema malengo na maswali ya utafiti wake.

2.4 Pengo la Utafiti

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu uhalisiajabu pamoja na kazi za fasihi za mwandishi Muhamed Said Abdulla. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Waliaula (2006), Wanjiru (2013), Abdalla (2015), Ibrahim (2016), na Mkindi (2016). Kupitia kazi hizo mtafiti amegundua kuwa bado hakujafanyika utafiti wenye kubainisha na kuchambua uhalisiajabu katika riwaya teule ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu na Mwitiko wa msomaji. Hivyo basi mtafiti ameona kuwa kuna pengo kubwa ambalo litahitaji kuzibwa katika uwanja wa fasihi wa Kiswahili. Kupita utafiti huu, mtafiti amekusudia kuliziba pengo hilo kwa kuchunguza uhaliajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

2.5 Mkabala wa Kinadharia

Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu dhana ya nadharia, miongoni mwa wataalamu hao ni Msokile (1993)anasema kuwa nadharia ni mawazo, mpango, utaratibu, sheria zilizowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Njogu na Chimerah (1999) wanafasili kuwa nadharia za uhakiki wa fasihi ni miongozo inayomsaidia msomaji wa kazi ya fasihi kuifafanua kazi ile kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na uchunguzi wa aina mbalimbali za fasihi. Wamitila (2002) naye anasema kuwa nadharia ni muongozo anaouendekeza msomaji na mhakiki wa kazi ya fasihi kupitia vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia.

Kwa ujumla mtafiti alihitimisha kwa kusema kuwa nadharia ni mpango, utaratibu au mwongozo unaomsaidia msomaji wa kazi za fasihi kuifafanua na kuichambua kazi yake. Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu/Uhalisia mazingaombwe katika lengo mahususi la kwanza na nadharia ya Mwiitiko wa Msoamaji katika lengo mahususi la pili. Mtafiti aliziteua nadharia hizi akiamini kwamba zimefanikisha kuyafika malengo ya utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza Uhalisiajabu katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale*. Hivyo basi katika sehemu ifuatayo nadharia ya Uhalisiajabu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo.

2.5.1 Nadharia ya Uhalisiajabu

Dhana yanadharia yauhalisiajabuimefasiliwa na wataalamu mbalimbali, kwa mfano: Mbatiah (2002) ambaye anaeleza kuwa istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasiahusawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kama kwamba ni mambo ya kawaida.

Kwa upande wa Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa uhalisiajabu ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelezwa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Wamitila (2003) anafasili kuwa uhalisiaajabu ni matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja ili yaonekane kama ya kawaida tu.

Kwa ujumla uhalisiajabu ni jumla ya visa, matukio au mambo yanayotokea katika jamii ambayo yanakiuka uhalisia. Matukio haya huweza kukiuka sifa na uwezo wa mwanadamu katika kuyatenda hayo.

2.5.1.1 Waasisi wa Nadharia ya Uhalisiajabu

Baadhi ya kauli za wataalamu ambazo zinazungumzia juu ya muasisi wa nadharia ya uhalisiaajabu ni kama vile Wamitila (2003) ambaye anaeleza kuwa muasisi wa nadharia ya uhalisiaajabu ni Franz Roh katika mwaka 1920. Aidha Warnes (2006) anadai kuwa muasisi wa nadharia hii ni Fridrich Freiherr von Hardenberg (Novalis) mwanzoni mwa karne ya 20.

2.5.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu

Kutokana na kazi za Danow (1995), Zamora (1995),Cooper (1998)na Encarta Encyclopedia (2002),wameeleza kuwa baadhi ya mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu nio hii ifuatayo:

i. Matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya.
ii. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.
iii. Mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, maana yake ni kuwa wana uhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.
iv. Wakati na mahali zina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine.
v. Uhalisiajabu umefungamana na sanaa jadi kama vile visasili. Visasili ni hadithi zinazoeleza asili ya watu na matukio fulani.

vi. Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Mtindo wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili.

vii. Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa.

viii. viii.Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu.

ix. Uhalisiajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbalimbali kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana.

Nadharia hii ilitumika kwa ajili ya kufanikisha lengo la kwanza la utafiti huu. Aidha mtafiti alitumia baadhi ya mihimili ambayo ilioana na kazi yake katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu kulingana na mada ya utafiti: *Kuchunguza Uhalisiajabu katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale*.

2.6 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007) wanaifafanua nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kwa kusema kwamba iliasisiwa na James na wenzake katika miaka ya 1960-1970. Waasisi hawa ni Wajerumani, ambao kwa pamoja wanaona kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake na si

kutokana na uzoefu wa mwandishi. Njogu na Wafula wanawaweka wafuasi wa nadharia hii katika makundi matatu. Makundi hayo ni kama yafuatayo:

i. Wale wanaoangazia kwenye tajriba za kipekee za msomaji. Hawa ni pamoja na C. C. Lewis, Stanley Fish na NormanHolland ambao walikuwa Wamarekani.
ii. Wale wanaofanya majaribio ya kisaikolojia kwa kikundi maalumu cha wasomaji. Hawa ni Reuven Tsur, Richarad Gerring, David Miall na Donald Kuiken
iii. Wale wanaochukulia kwamba wasomaji wote wa kazi ya fasihi wataipokea kwa njia iliyo sawa.

Katika kushadadia nadharia hii Njogu na Wafula (2007)wanasema kwamba Stanley Fish anadai kwamba sanaa ya maneno haichanganuliwi kwa kutumia mikakati ya jaribio la kisayansi. Anayefanya jaribio la kisayansi huweka mpaka wa kihisia na kimawazo kati ya nafsi yake na jambo linalomshughulisha. Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira. Kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja.

Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi yoyote ya sanaa hurejelea kazi inayosomwa kwa fasili ili ithibitishwe kuwa kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji wa kazi ya fasihi. Aidha, hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

2.6.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007)wanasema wananadharia ya Mwitiko wa Msomaji huuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejiegemeza. Maswali hayo ni kama haya yafuatayo:

i. Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?
ii. Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na namna anavyoichukulia?
iii. Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.
iv. Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Kinoti (2012) anamnukuu Adena Rosmarin katika Murfin (1999) anaeleza kwamba kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo, Kinoti anaibainisha mihimili ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatayo:

i. Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kwa kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela. Iser na Fish (1980) katika Njogu na Wafula (2007), wanadai kwamba kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hushurutika kutunga matini mpya ambazo zimechochewa na kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa.

ii. Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi. Wasomaji hufasiri athari hizo kupitia njia tofauti tofauti kutegemea:
   a. Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.
   b. Namna matini inavyoelekeza au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa inayozua usomaji mzuri ama mbaya wa kazi ya fasihi.

iii. Wananadharia hii wanashikilia kuwa kuna njia mbili za usomaji wa kazi za fasihi ambazo ni:
   a. Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejuilikana na kutambuliwa na msomaji.

   b. Kuwasilisha kazi ya fasihi kimafumbo ili kumchochea msomaji kujitafutia na kujiamulia ujumbe uliomo katika kazi aliyoisoma. Kwa hivyo, mafumbo hayo yanapaswa kusomwa na msomaji mara kadhaa ili kupata ujumbe uliokusudiwa.

iv. Usomaji ni tendo linalofanywa na kutekelezwa na msomaji kwa wakati maalumu, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri maana ya matini hiyo.

v. Msomaji anayetumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hufuata hatua tatu, nazo ni:
   a. Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.

b. Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.
c. Hudhihirisha maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.

vi. Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi.

2.6.2 Upungufu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Salim (2015) anasemanadharia ya Mwitiko wa Msomaji inaelezwa kuwa na mapungufu kutokana na kuiona kazi ya fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji. Kwa mantiki hiyo, msomaji asiyekuwa makini anaweza kuipa kazi husika maana finyu.

Pamoja na upungufu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti aliamini kwamba nadharia hiyo iliwezesha kuzihusisha dhamira zinazoibuliwa na vipengele vya uhalisiajabu na uhalisia wa maisha ya kijamii. Hivyo basi, mtafiti aliona kuwa hii ni nadharia muafaka katika kufanya uchambuzi wa lengo mahususi la pili la utafiti huu ambalo linahusu dhamira zinazojitokeza kupitia vipengele vya Uhalisiajabu.

2.7 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefanya mapitio ya kazi tangulizi kuhusu vipengele kadhaa vinavyohusiana na mada ya utafiti. Sura hii imeanza kwa utangulizi na kuendelea kuelezea dhana ya uhalisiajabu na dhamira. Vile vile, sura hii imetalii maandishi kadhaa kuhusu riwaya za Mohamed Said Abdulla kwa nia ya kubainisha pengo la utafiti lililoshughulikiwa katika utafiti huu. Mapitio haya yameonesha kuwa hakuna mtafiti aliyewahi kufanya utafiti kwa nia ya kuchunguza vipengele vya uhalisiajabu

na namna vipengele hivyo vinavyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Kutokana na ukweli huo mtafiti aliona kuwa kuna nafasi ya kufanya utafiti ili kuziba pengo hilo la kitaaluma. Sura hii pia imefanya uchambuzi wa nadharia ya Uhalisiajabu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambazo zimeongoza utafiti huu. Mwisho, sura hii imetoa hitimisho. Sura ifuatayo inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni njia na taratibu zote zinazopaswa kufuatwa wakati wa ukusanyaji wa data (taarifa) kulingana na aina ya utafiti (Enon, 1998). Sura hii ilihusisha vipengele muhimu vinavyohusiana na mbinu pamoja na njia za utafiti. Miongoni mwa vipengele vilivyoongelewa kwenye eneo hili ni kama vile: Eneo la utafiti, mbinu za utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data, mbinu za ukusanyaji wa data pamoja na hitimisho.

3.2 Eneo la Utafiti

Dhana ya eneo la utafiti imejadiliwa na wataalamu mbalimbali, kwa mfano: Creswell (2009) anaeleza kuwa eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyika kulingana na vile mtafiti alivyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti. Hivyo basi eneo la utafiti huu ni Maktabani.Maktaba ambazo utafiti huu ulifanyika ni pamoja na maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) katika tawi lake lilioko Chakechake Pemba, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), iliyoko Mchanga mdogo, Wete Pemba na Maktaba Kuu Zanzibar iliyoko Chachani, Mjini Chake chake. Maktaba nyengine zilizotumika ni maktaba ya Kituo cha Walimu Michakaeni Chake Chake Pemba**.** Mtafiti amechagua maeneo haya kutokana na urahisi wa kukusanya data za utafiti na upatikanaji wa marejeleo anayoyahitaji kwa wepesi.

3.3 Kundi Lengwa

Wataalamu kadhaa wamefasili maana ya kundi lengwa, miongoni mwa wataalamu hawa ni Kombo na Tromp (2006) ambao wameeleza kwamba kundi lengwa ni jumla

ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Pia kundi lengwa ni kundi la watu au vitu linalofikiriwa kuwa na sifa na vigezo vinavyowawezesha kuteuliwa kwa ajili ya uchunguzi; kundi hili hudhaniwa kuwa na taarifa muhimu zinazohitajika kuhusu jambo linalokusudiwa kuchunguzwa. Hivyo katika utafiti huu kundi lengwa ni ni riwaya zote za Mohamed Saidi Abdulla.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu dhana ya sampuli: Mligo (2012) anafasili kwamba sampuli ni kundi fulani la watu (vitu) lililomo ndani ya mkusanyiko wa watu (vitu) ambalo mtafiti anaamini kwamba lina habari zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti, kama vile kundi la walimu nakadhalika. Aidha Prewitt (1996) anatilia mkazo mawazo hayo kuwa sampuli hutumika kutoa taarifa zinazochunguzwa na mtafiti.

Sambamba na hayo, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa (Sigh, 2007).Pia sampuli ni jambo muhimu katika utafiti kwa sababu ni hatua ya kufikiaukusanyaji wa data za utafiti kulingana na mada husika. Kutokana na hayo sampuli aliyoichagua mtafiti ni sampuli lengwa.

3.4.1 Sampuli Lengwa

Fasili ya sampuli lengwa imeelezwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao ni Yin (1994) anasema kuwa sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti anateuwa watafitiwa ambao watampatia data zitakazoweza kufanikisha malengo ya utafiti wake.

Katika utafiti huu mbinu hii ya sampuli lengwa ilitumika katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambapo mtafiti alishughulikia uhalisiajabu ulivyojitokeza katika riwaya hii. Aidha mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi kwa vile mtafiti alifanya utafiti wake kwa kuzingatia sampuli lengwa tu kulingana na malengo pamoja na maswali ya utafiti wake.

3.5 Aina za Data

Baadhi ya wataaalamu wamefasili data kuwa ni maelezo au ukweli unaopatikana kwa kutumia uchunguzi maalum au majaribio (Robnson, 1996). Pia data ni maelezo yenye ukweli yanayotumika kama ni kiini cha sababu, majadiliano au majumuisho (Allen, 2004). Kuna aina kuu mbili za data ambazo ni data za awali na data za upili. Katika kushadidia hayo, Panneerselvam (2012) anaeleza kuwa data zimegawika katika makundi mawili ambapo anaona kuwa kuna data za msingi na data za upili. Katika utafiti huu data zilizokusanywa ni data za awali na data za upili.

3.5.1 Data za Awali

Dhana ya data za awali imeelezwa na wataalamu tofauti tofauti wa utafiti akiwemo Panneerselvam (ameshatajwa) anaeleza kuwa data za msingi ni zile ambazo hukusanywa na mtafiti uwandani. Data hizi kwa kawaida hukusanywa kwa matumizi ya sasa na baadaye. Aidha data za msingi ni data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kutoka katika eneo alilolichagua kwa ajili ya matumizi ya utafiti wake kulingana na mada ya utafiti. Data za msingi katika utafiti huu zilitokana na riwaya teule ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kupitia mbinu ya Usomaji makini maktabani.

3.5.2 Data za Upili

Wataalamu mbalimbali wamejadili kuhusu dhana ya data za upili, miongoni mwao ni Kothari (2004) ambaye anasema kuwa data za upili ni data zote ambazo tayari zimekwishakusanywa na watafiti wengine na ambazo zimepitia katika hatua zote stahiki za ukusanyaji wa data. Data za upili ni data zote zinazopatikana kutoka vyanzo tangulizi au data zilizokusanywa na watu wengineo kwa malengo maalumu. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia data za upili kwa lengo la kushadidia na kutilia mkazo taarifa alizozipata kutoka katika data za awali. Katika utafiti huu, mtafiti amesoma kwa umakini kazi tangulizi mbalimbali kama vile tasnifu, vitabu, makala, majarida magazeti, ripoti na wavuti mbalimbali ambazo zimehusiana na mada ya utafiti kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka.

3.6 Ukusanyaji wa Data

Wataalamu mbalimbali wameeleza maana ya ukusanyaji wa data. Miongoni mwao ni Kombo na Tromp (2006) na Kothari (2008)wamefasili kuwa ukusanyaji wa data ni njia na zana zitumikazo katika kukusanya taarifa za kiutafiti katika kutolea majumuisho. Ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti.

3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data imefasiliwa na wataalamu kadhaa wakiwemo Kothari (1990)ambaye anaeleza kuwa mbinu za ukusanyaji data ni njia anazochagua mtafiti kuzitumia kukusanya data kwa ajili ya utafiti wake. Utafiti huu umekusudia

kukusanya data zake kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa riwaya teule ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

3.6.2 Mbinu ya Usomaji Makini

Dhana hii imejadiliwa na wasomi na wataalamu kadhaa, miongoni mwao ni Enon (1998) anafasili mbinu ya usomaji makini kwamba ni mbinu inayomtaka mtafiti kukusanya taarifa kwa umakini baada ya kusoma kwa kina kazi husika kuanzia mwanzo hadi mwisho. Aidha katika mbinu hii ya usomaji makini mtafiti husoma kazi hizo tena na tena mpaka pale atakapojiridhisha kuwa sasa amepata data za kutosha ambazo zitakidhi na kuweza kukamilisha malengo ya utafiti wake.

Kupitia riwaya teule ya *Mzimu wa Watu wa Kale* na mapitio ya kazi tangulizi, mtafiti ametumia mbinu ya usomaji makini kwa lengo la kupata data za awali/msingi za utafiti kulingana na malengo ya utafiti wake na baadae kuweza kuzichambua data hizo ipasavyo.

3.6.3 Mbinu ya Upitiaji Nyaraka

Wataalamu kadhaa wamejadili juu ya dhana ya mbinu ya upitiaji nyaraka. Miongoni mwao ni Kothari (1990)ambaye anasema kuwa mbinu ya upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti, kukusanya machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa umakini. Mtafiti amekusudia kusoma au kuzipitia kwa umakini makala, ripoti, tasinifu, majarida, vitabu, wavuti na tovuti pamoja na nyaraka nyenginezo muhimu ambazo zimehusiana na mada ya utafiti wake ili kupata data za upili zenye uhakika kwa matumizi ya utafiti wake na kwa kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti.

3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo kubalifu na muhimu ambacho mtafiti hukifanya mara baada ya kukusanya data za utafiti kutoka katika vyanzo husika kwa lengo la kupata uhalali wa tarifa husika za utafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi wa data ili kupata matokeo sahihi ya utafiti wake pamoja na kufanikisha malengo ya utafiti huo.

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

Wataalamu mbalimbali wamejadili kuhusu dhana ya mkabala wa kimaelezo miongoni mwao ni Kothari (1990), ambaye anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Mbinu hii hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi kwa sababu fasihi ni taaluma ya maneno ambayo kuandikwa au kuzungumzwa. Aidha mkabala wa kimaelezo ndiyo mbinu ya uchambuzi wa data zilizokusudiwa kutumika katika utafiti huu ambayo iliongozwa na nadharia ya uhalisiajabu. Mkabala huo umetumika kwa kiwango kikubwa, wastani wa asilimia 80%. Mbali na hayo mkabala wa Kitakwimu ulitumika kwa kiwango kidogo; wastani wa asilimia 20% ya utafiti huu kwa lengo la kushadidia na kufanya muhtasari wa utafiti huu katika uchambuzi wake.

3.8 Hitimisho

Sehemu hii imeeleza mbinu za utafiti na vipengele vyake ambavyo mtafiti amevitumia katika kuuendea utafiti wake. Vipengele hivyo ni pamoja na eneo la utafiti, mbinu za utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data, mbinu za ukusanyaji wa data pamoja na vifaa vya kukusanyia data na hitimisho. Katika

sehemu hii kila kipengele kina umuhimu wake katika kukamilisha utafiti huu ili kufanikisha malengo yake na kujibu maswali kwa kiwango kilicho bora. Aidha, sehemu hii ni miongoni mwa sehemu muhimu na ni dira ya utafiti huu kwa vile kila kipengele kimeelezea mambo muhimu yanayohusiana na utafiti huu. Sura ifuatayo ilishungulikia uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizopatikana katika utafiti huu kuhusiana na mada ya utafiti. Utafiti huu ulilenga kuchunguza vipengele vya uhalisiajabu na namna vilivyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Sura hii imefanya uwasilishaji wa vipengele vifuatavyo: Usuli wa mwandishiMohamed Said Abdalla na muhtasari wa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Vile vile, sura hii imefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data zinazohusu vipengele vya uhalisiajabu ambavyo vililenga kujibu swali lakwanza la utafiti huu. Baada ya uwasilishaji huo mtafiti alifanya uchambuzi wa data zinazohusu namna vipengele vya uhalisiajabu vinavyoibua dhamira katika riwaya teule. Alifanya hivi ili kujibu swali la pili la utafiti. Mwisho sura imemaliza kwa kueleza hitimisho.

4.2 Usuli wa Mwandishi: Mohamed Said Abdulla

Abdalla na wenzake (2014) katika *Kanzi ya Wanariwaya* wanaeleza kwamba Muhammed Said Abdullani mwandishi wa vitabu mbalimbali vya fasihi ya Kiswahili aliyezaliwa mnamo tarehe 25/4/1918 huko Makunduchi Zanzibar. Alikuwa na ukaribu sana na wageni wa Kizungu (enzi hizo za Wakoloni). Wageni hao ndio waliompatia elimu yake kutoka katika shule ya kimishionari na akamalizaelimu ya sekondarimnamo mwaka 1938.

Pia, alifanikiwa kuoa mke mmoja na akapata watoto wawili, ambao walipoteza uhai wao katika mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwaka 1964. Hii ilikuwa kumbukumbu

isiyofutika katika uhai wake. Nguli huyu wa ubunifu na uandishi wa riwaya za upelelezi alifariki mwaka 1991.

Baada ya kumaliza kisomo chake cha sekondari alifanya kazi katika Kitengo cha Afya cha Serikali ya Kikoloni. Baada ya miaka kumi aliamua kujiingiza katika Uandishi wa habari. Mwaka 1948 alikuwa mhariri wa gazeti la Zanzibar pia amewahi kufanya kazi kama mhariri msaidizi wa magazeti ya *Al falaq*, *Al mahda* na *Afrika Kwetu*. Mwaka 1958 akawa mhariri wa *toleo maalumu la taifa la kilimo* (Zanzibar) kazi aliyoifanya mpaka alipostaafu mwaka 1968.

Muhammed Said Abdulla alifahamika sana katika eneo la Afrika mashariki. Hii ilitokana na utunzi mzuri wa kazi zake zilizowavutia na kuwasisimua wengi zenye visa na mikasa. Pia aliwavutia wasomaji wake kutokana na matumizi makubwa ya lugha ya Kiswahili pamoja na mitindo anuai ya kifani iliyojenga ubora wa kazi zake. Hali hii ilipelekea baadhi ya kazi zake kutumika katika shule kama vitabu rejea vya fasihi ya Kiswahili.

Alitunga riwaya za aina mbalimbali zilizohusishaupelelezi, ujasusi nahata mambo ya kijamii. Riwaya zake kwa idadi zinafika saba (7) ambazo ni*Mzimu wa Watu wa Kale* iliyochapwa naE.A.L Nairobi mwaka 1960, mwaka 1968 alitoa iitwayo*Kisima cha Gining*iliyochapwa na Evans Brother’s Nairobi. Mwaka 1974 alitoa riwaya mbili ambazo ni *Siri ya Sifuri* na *Duniani Kuna Watu* zilizochapwa na East African Publishing House. Mwaka 1975 alitoa *Mke Mmoja Waume Watatu,Mwana wa Yungi Hulewa*zilizotumgwamnamo mwaka 1976 na kuchapwa na East African PublishingHouse.Riwaya iliyofunga ukurasa katika utunzi wake ni*Kosa la Bwana Msa*iliyotolewa mnamo mwaka 1984 nakuchapwa na East African Publishing House.

Muhammed Said Abdulla pia alikuwa na kazi nyingine za fasihi nje ya riwaya. Kazi hizo zipo katika utanzu wa hadithi fupi. Mfano, kuna hadithi iitwayo*Mke Wangu*ambayo kwa ufupi inajaribu kuzungumzia mhusika mmoja wa kiume tajiri wa mjini. Tajiri huyo alikuwa akimhusudu binti mmoja wa hali ya kawaida sana, ambaye alitaka amuoe na amuweke katika hali kama aonekanavyo yeye. Lakini baadaye alikuja kugundua kuwa binti yule alikuwa na haiba ya pekee na alijitambua vyema. Pia alikuwa si wa kujirahisisha kwa kila mtu, vilevile mtunzi huyu aliandika*Insha*zilizochapishwa katika toleo lililoitwa*Uandishi wa Tanzania*.

Maudhui ya kazi zake nyingi yamelenga katika kuifumbua jamii kutokana na mambo kadha wa kadha yanayoitatiza. Maudhui ya kazi zake kwa ujumla ni ya kimapinduzi mfano. Katika riwaya ya*Siri ya Sifuri* na *Kosa la Bwana Msa*maudhui yake (dhamira) ni upelelezi. Pia katika*Mzimu wa Watu wa Kale*maudhui yake ni upelelezi na athari ya dhuluma, ukoloni na kadhalika. Katika riwaya ya*Duniani Kuna Watu*dhamira zakeni upelelezi,maadili na maonyo kwa binadamu. Pia katika*Mwana wa Yungi Hulewa*dhamira yake ni mila na tamaduni mbalimbali za Kitanzania.

Bwana Muhammed Said Abdulla alikuwa ni mwandishi mwenye kujitofautisha sana na waandishi wengine, hasa katika ujenzi wa fani katika kazi zake mbalimbali. Aliweza kujenga kazi zake kwa vipengele tofauti ambavyo vilizifanya ziwe na upekee. Mfano katika*Mzimu wa Watu wa Kale*aliwajenga wahusika wake waonekane ni wenye kauli na matendo ya kuaminika sana, katika uga huohuo wa wahusika pia imeonekana jinsi gani alivyoweza kuwapa wahusika wake majina yenye kuleta hisia/taswira pindi jina linapotamkwa. Mfano katika*Siri ya Sifuri*kuna mhusika anaitwaWasiwasi Malifedhahii inaashiria kuwa huyu alikuwa tajiri wa mali na fedha,

kuna mwingine anaitwaHafifu Mfukohii inakupa picha kuwa huyu hakuwa tajiri. Katika*Mwana wa Yungi Hulewa*kuna mhusika anaitwaTwajuanaambaye ni kijakazi, Pia katika*Kosa la Bwana Msa*kuna mhusika mwanamke tajiri anaitwaShinunahivyo sasa tunaona jinsi alivyoumba wahusika wake kwa majina yenye taswira fulani.

Pia kuna usawiri makini wa mandhari aliyoyachagua, mfano kuna maeneo kama Unguja, Pemba na baadhi ya maeneo ya Tanga na Dar es Salaam yakionesha maisha ya Waarabu walioishi mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki na kujifunza Kiswahili kwa wenyeji au Waswahili. Mbali na hayo kuna matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili yenye mnato na hisia, pia umbuji wake uliendelea kuonekana pale alipotumia lugha ya Kiingereza na lafudhi ya Kiarabu katika kuwakilisha wahusika na uhusiano wao ili kuleta mvuto kwa wasomaji.

4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale

Riwaya ya *Mzimu waWatu wa Kale* ni riwaya ya upelezi iliyoandikwa na Mohamed Said Abdulla na kuchapishwa kwa mara ya kwanza E.A.L Nairobi mwaka 1960. Riwaya hii inaeleza kuhusu *Mzimu wa Watu wa Kale* ambao ulikuwa una vitisho vya aina kwa aina kwa watu waliokuwa wameuzunguka. Iliaminika kuwa katika mzimu huo kulikuwa na mizimu ambayo ilikuwa ikitoka katika msitu huo na kuwaendea watu waliokaribu na mzimu huo na kuwahangaisha huku wakiwa wamelala. Kutokana na hali hiyo watu wengi waliendelea kuuogopa na kutii masharti ya mzimu huo ikiwa ni pamoja na kupiga hodi wakati mtu anapotaka kupita.

Mhusika mkuu katika riwaya hii ni Bwana Msa ambaye anaambatana na Najim katika motifu ya msako ya kumtafuta mtu aliyemuua Bwana Ali. Huu ni msako wa

upelelezi unaofanywa na Bwana Msa mtu ambaye si polisi akimuongoza Najim na Inspekta Seif ambaye ni askari polisi. Cha kushangaza ni kwamba Bwana Msa anafanikisha kutambulika kwa mtu ambaye alimuua Bwana Ali baada ya kufika kwa Banyani na kumtaka aeleze kuhusu stakabadhi na atoe pesa alizokuwa awe nazo Bwana Ali baada ya kumuuzia shamba. Yote hii ilitokea baada ya Bwana Msa kushangazwa na stakabadhi ambayo haikuwa na saini wala tarehe.

Kwa ujumla lengo mahasusi la pilim la kazi hii linaibua dhamira mbalimbali zinazoihusu jamii kwa mbinu ya Uhalisiajabu. Dhamira kuu inayojadiliwa katika riwaya hii ni mauaji kama yanavyofanywa dhidi ya Bwana Ali. Masuala mengine yanayojadiliwa na msanii ni pamoja na imani za jadi, uongozi mbaya, ukoloni, utabaka, mauaji, umuhimu wa kutunza kumbukumbu, upelelezi, uganga, unyonyaji na ukandamizaji pamoja na nafasi ya mwanamke.

4.4 Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale

Riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ni riwaya ya Kiswahili ambayo imechota ujumi wa matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu kama sehemu ya bunilizi katika kuibua dhamira za mtunzi. Vipengele hivyo vya kiuhalisiajabu vimefumwa na msanii vikiwa vimekiuka uhalisi wa kijamii. Hivyo basi, katika sehemu hii utafiti huu ulifanya uchambuzi na kuwasilisha data zinazohusu vipengele vya uhalisiajabu kama vinavyojidhihirisha katika riwaya teule.

4.4.1 Usawiri wa Wahusika wa Kiuhalisiajabu

Wahusika katika kazi ya fasihi ni viumbe wa sanaa ambao hutumiwa katika kazi hiyo. Wataalamu wengi wametoa fasili zao kuhusu maana ya wahusika. Miongoni

mwa wataalamu hao ni Wamitila (2002) ambaye ameeleza kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Wahusika hao huweza kuwa binadadamu, wanyama au viumbe vyengine ambavyo hutumiwa na msanii ili kuwakilisha tabia na sifa za watu waliomo katika jamii.

Aidha, Wamitila (2013) anaeleza kuwa kuna wahusika wa kiuhalisia na wa kiuhalisiajabu. Kuhusu wahusika wa kiuhalisia anafafanua kuwa ni wale wahusika wanaofuata misingi ya kiuhalisia na matendo wanayotenda ni matendo au matukio ya kawaida ambayo hayana elementi za mazingaombwe au maajabu. Kwa upande wa wahusika wa kiuhalisiajabu ni wale ambao wanaohusishwa na visasili, njozi au fantasia na matendo yao hayafuati kanuni wala sharia za maisha ya kawaida. Pia wanakuwa na sifa ya kutodadisi misingi ya matukio ya kimazingaombwe ambayo yanautawala ulimwengu wao. Wamitila (ameshatajwa) anampigia mfano mhusika msimulizi wa hadithi katika riwaya ya *Mzingile* ambaye haelekei kudadisi kudenguliwa kwa dhana nzima ya kiwakati.

Pamoja na hao Wamitila (ameshatajwa) anasema kuwa kuna uwezekeno wa wahusika wa ulimwengu wa wafu kuingiliana moja kwa moja na wahusika wanaopatikana katika ulimwengu wa wanaoishi. Kwa mfano wahusika Marx, Fred na wengine katika riwaya ya Nagona wanajitokeza kushiriki katika Ngoma kuu. Hivyo riwaya hizi huwa huru kwa vile hutumia mawanda mapana ya kibunilizi.

Data zilizokusanywa katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* zinaonesha kuwa mwandishi ametumia wahusika wa uhalisiajabu. Kwa mfano, mwandishi amemchora muhusika Kipwerere akiwa ni mhusika anayeibua maajabu. Kipwerere ni binadamu

lakini katika hadithi hii inasimuliwa kwamba alikuwa na uwezo wa kutambua mambo ambayo yatatokea baadae kinyume na hali ilivyo kwa binadamu wa kawaida. Hata pale anapopata ajali na kujeruhiwa vibaya hajali. Msanii anasimulia hivi:

> Baada ya muda kitambo muwele, alianza kuharakisha kichwa chake kidogo kidogo, na baadae akaanza kutika na kuzungumsha kichwa huku na huku, mpaka kikashika kasi-shetani tayari kichwani. Kipwerere alizuka pale alipokaa akamsukuma mama yake chini, yeye akajitupa chini kwa nguvu sana, kichwa chake kikafika juu ya ncha ya ukingo wa baraza, akapiga siyahi ya nguvu sana kisha akainuka hali damu zinamtoka kichwani…Kipwerere, taratibu kama siye, aliondoka pale chini, damu zinamchiririka usoni kama mfereji, akarudia msalani kwake, akakaa tena kama alivyokuwa kwanza, amenyoosha miguu upande wa kibla na kumuashiria mama yake ambaye sasa hivi amekwisha jizoazoa pale chini aliposukumwa, aje kumfunika tena (uk. 11).

Kupitia dondoo hili msanii anaonesha namna mhusika Kipwerere alivyosawiriwa, kutokana na tabia yake ya kufanya matendo yake ya kiajabuajabu yenye kukiuka uhalisia. Kwa mfano, Kipwerere alimsukuma mama yake na kumuangusha chini na baadaye anapasuka kichwani na kutoka damu kwa wingi lakini hajali kwa tukio hilo. Mtafiti amebaini kwamba mhusika huyu ni wa kiuhalisiajabu kama ilivyoeleza Wamitila (2013) hapo kabla, kwamba matendo ya wahusika wa kiuhalisiajabu hayafuati kanuni za maisha ya kiuhalisia.

Kipwerere analandana na nadharia ya Uhalisiajabu ambapo moja ya msingi wa nadharia hii kama inavyoelezwa na Njogu na Wafula (2007) ni kuwa katika kazi za kihalisiajabu matukio yasiyokuwa ya kawaida hufumwa na kuelezwa kama matukio ya kawaida lakini huwa yamekiuka ulimwengu wa kiuhalisia.

Pia, Shetani ni mhusika mwengine aliyechorwa kiuhalisiajabu katika riwaya hii ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Shetani ni kiumbe asiyeonekana na binadamu. Hata hivyo

katika riwaya hii msanii alisimuliwa kuwa shetani anaingia katika mwili wa Kipwerere na kumfanya awe hajitambui huku akieleza maneno ambayo yanaibua maajabu kwani hatimae yalitokea kuwa ya kweli. Tukio hili linasimuliwa na msanii wakati Kipwerere alipopagawa na shetani. Msanii alisimulia kwa kusema:

> "…Alipokwisha funikwa, shetani alianza kutika na kuzungumsha kichwa kwa nguvu sana, kisha akasema, "Nimeona! Nimeona! Kiza! A-aaa! Hapana kitu! Safi kabisa! Hapana kitu! Nyekundu –u!..." (uk 11)

Dondoo hili linaonesha namna Kipwerere alivyoongozwa na Shetani ili kuagua matukio yaliyompata Bw. Ali. Hizi ni nguvu za kiza ama baadhi ya watu wanaziita nguvu za kisihiri ambazo kuaminika kwake bado hadi sasa haziwezi kuthibitishwa kwa misingi ya Kisayansi. Hata hivyo hadi sasa pamoja na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia wapo wanajamii katika kila pembe ya dunia wanaoamini nguvu hizi.

Tukio hili pia linawiana na nadharia ya Uhalisiajabu. Hili ni tukio la kinjozi na lililokiuka ushabihi kweli. Kama asemavyo Wamitila (2013) kwamba matukio ya kihalisiajabu hukiuka ushabihi kweli wa maisha ya ya kijamii. Ambapo matukio yanayokiuka uhalisia wa maisha ya kawaida hufumwa na kama matendo ya kawaida. Matukio kama haya ndio mtafiti aliyokutana nayo katika hadithi kama vile ya *Nagona* ya Kezilahabi ambapo mhusika anakuwa na mguu mrefu ambao anapounyoosha unafika upande mwengine wa bahari.

Katika Riwaya ya mzimu wa watu wa kale muhusika mwengine wa uhalisiajabu ni mama Kipwerere. Ambaye amechorwa akiwa na nafasi ya mzee na nafasi ya mganga wa jadi anayemhudumia mwanawe. Haya yamebainika katika nukuu zifuatazo:

> Aliingia ndani chumbani akampa habari mwanawe kuwa sasa ni kushikwa sikio. Kipwerere alijizoazoa pale kitandani alilipolala akatangulia uani; mama mtu alifungua kisanduku akatoa kanga mbili za kwenda kumfunika muwele. Alimkuta muwele amekwisha kukaa juu ya mswala na miguu yake ameinyoosha upande wa kibla. Mama Kipwerere alimfunika mwanawe kanga zote mbili gubigubi, tangu kichwani mpaka nyayoni, naye akarudi na kazi yake ya kutengeneza moto na manukato ya kumfukizia. Katika kifurushi kilichikuwa karibu yake alitowa pachori na pakanga, udi na ubani wa makaburini, kusti na mea, alipokwisha vitia vyote hivi pamoja katika moto, alisogea akapenyeza mkono kile kitezo kinachotowa biwi la moshi linalonuka na kunukia pamoja, akimzungushia mwanawe kichwani na huku akiomboleza kwa maneno yenye lafudhi au matamko kama Kiswahili cha Pemba cha ndani au Kiswahili cha asili cha Makunduchi; lakini la mimi wala wewe hatukufahamu.
>
> Bi Kazija mama yake Kipwerere, anafahamu maneno ya shetani wa mwanawe, na kaagua kuwa kuna jambo baya mbele yao linakuja-jambo kama la kifo- na kafara lake linataka mbuzi mwekundu achinjwe ‘waruke damu’ (uk. 13).

Kutokana na dondoo hii mama Kipwerere amesawiriwa kuwa ni muhusika anayefanya mambo ya kiajabu ambayo yamekiuka maisha ya uhalisia. Matendo kama haya yanaonekana yakitendwa na baadhi ya waganga wa jadi ambapo kiukweli hayawezi kuthibitika kwa misingi ya kisayansi katika jamii. Mbali na hayomama Kipwerere ni mjuzi wa lugha ya mashetani ambayo ni vigumu kuelewa watu wengine. Hii ni kutokana na manuwizi yake na kuweza kufumbua fumbo la shetani wa mwanawe na kutaja kafara lake.

Kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu ni wazi kuwa tukio hili linaendana na nadharia hii. Njogu na Wafula (2007)wanasema kuwa matukio ya kiajabu na yasiyokuwa ya kawaida huonekana ni ya kawaida katika kazi za uhalisiajabu. Kutokana na hali hii ndio maana matukio anayoyafanya Bi. Kazija ya kuagua yale yanayotarajiwa kumpata mtoto wake yanachukuliwa ni matukio ya kawaida.

Wahusika wengine wa uhalisiajabu waliotumika katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ni maiti. Tunaelezwa kuwa watu waliokua wakiishi karibu na mzimu wa watu wa kale walikuwa wakijiwa na maiti usingizini. Maiti hao walikuwa hawana miili tena lakini walikuwa wakiwataabisha sana watu huku wakiwa wamelala. Msanii anatusimulia hili kwa kuusema:

> Mara nyingi wenyeji wa pale watakwambia wamejiwa na maiti hao usingizini hawana miili tena ila wamebakia vivuli tu; na wao huwataabisha sana walalapo. Mpaka uje wakati na wao waone ni mno tena, watu wote wa kiamboni-ila Bwana Ali hajapata kutoa kitu-wanunue ngombe na mapaji mengine watowe kafara la kuwatuliza mizimu ilale ili na wao wapate kutulia. (uk. 17).

Kutokana na dondoo hili utafiti umebaini kuwa wahusika hawa ni wa uhalisiajabu. Wahusika hawa huwafanyia wanakijiji vitendo vya kiajabuajabu wanapokuwa wamelala ili kuwatisha wasilale. Wanakijiji waliamini kwamba mateso hayo hayataweza kuondoka bila kushirikiana kutoa kafara la kuwatuliza mizimu hao.

Kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu mtafiti amebaini kuwa usawiri huu wa wahusika maiti wanaowatokea watu katika ndoto unalandana na nadharia ya uhalisiajabu. Kama asemavyo Wamitila (2013)kwamba katika kazi za uhalisiajabu uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu labda mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yupo ndotoni.

Vile vile, msanii amesawiri wahusika wengine wa uhalisiajabu ambao ni tumbili na makima wa mzimuni. Tumbili na makima hao walikuwa wakiharibu mazao ya watu lakini watu hawakuweza kuchukua hatua yoyote kwa imani kwamba huenda ikawa

ni vizuu wa watu saba wa kale. Kwa mantiki hiyo walikuwa na hofu ya kutowakera. Kuhusu hili msanii anatusimulia kwa kusema:

> Jinsi mzimu wa watu wa kale unavyotisha namna hii hata wale tumbili na makima walivyozaliana wakajazana ndani ya kichaka hicho, pindi wakigundulika wanaharibu konde za watu mashambani mwao, wenyeji wale hukataza wasipigwe, maana walisema kwamba huenda ikawa wanyama wale ni vizuu vya wale watu saba wa kale (uk. 17).

Kupitia dondoo hii mtafiti ameona namna tumbili na makima wa mzimuni wanavyoharibu vipando vya wanakijiji bila ya kuguswa kutokana na hofu, vitisho na woga ulivyojengwa kwa wanakijiji hao. Makima na tumbili ni wahusika wa uhaliajabu kutokana na kuwa matendo hayo ni kunyume na uhalisi. kwa vile hakuna tumbili wala kima anayeharibu mazao ya watu akaachiwa bila ya kuzuriwa.

Matumizi ya wahusika kima na tumbili kama inavyoelezwa katika sehemu hii yanawiana na nadharia ya Uhalisiajabu. Kuhusu matumizi haya mwandishi Wamitila (2013)anasema kuwa mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Hivyo basi wahusika manyani na kima ni mfano wa wahusika wanaojikita katika msingi huu.

4.4.2 Mandhari ya Kiuhalisiajabu

Mandhari ni mazingira, mahali, sehemu au wakati ambapo matukio, visa na mikasa ya kazi ya mwandishi au msanii inakusudiwa kufikishwa kwa jamii husika ili kusawiri na uhalisia wa maisha ya jamii hiyo. Wapo wataalamu mbalimbali ambao wameelezea dhana ya mandhari kwa kina katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Njogu na Chimerah (1999)wamefafanua maana ya mandhari kuwa ni mahali au

makaazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi na namna matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi yanavyotendeka.

Aidha, Madumulla (2011) anaeleza kwamba mandhari katika kazi za fasihi ni mahali ambapo tukio linatendeka. Mandhari katika kazi ya fasihi zinaweza kuwa za kidhahania au halisi. Pamoja na hayo, Kezilahabi (1983) amebainisha aina mbili za mandhari yaani mandhari ya kubuni na mandhari halisi. Pia anaeleza kuwa mwandishi anayetumia mandhari ya kubuni hana tatizo sana katika kuchagua mandhari yanayofaa katika kazi yake. Kwa mfano, katika simulizi za visasili mwandishi hudokeza uhalisiajabu kwa namna fulani ili kuonyesha kwa makusudi kuwa mwanadamu si mjuzi wa maarifa yote. Aidha kwa mwandishi anayetumia mandhari halisi huwa anakabiliwa na tatizo kubwa. Hii ni kutokana na kuwa mandhari anayoichagua lazima ibebe sura halisi ya kile kinachosimuliwa.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* data zinaonesha kuwa kuna matumizi ya mandhari ya uhalisiajabu. Mandhari haya ni yale ambayo yamekiuka uhalisia ambao tunakutana nao katika kazi mbalimbali za fasihi ambazo zimesaniiwa kwa mbinu za kihalisia. Mandhari ya uhalisiajabu yanajitokeza zaidi kupitia mzimu wa watu wa kale. Hivyo basi, baada ya kuzichambua data zilizokusanywa kutoka riwaya teule ilibainika mandhari haya yanajitokeza katika kategoria ndogo ndogo zifuatazo:

4.4.2.1 Mandhari ya Kichaka cha Mzimu wa Watu wa Kale

Kwa kawaida kichaka ni sehemu inayotowa mahitaji muhimu katika maisha ya binadamu kama vile kuni, matunda, kivuli, miti na fito za kujengea. Kinyume na hayo kichaka kinachozungumzwa katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ni

mandhari ya uhalisiajabu ambayo inatuibulia maajabu. Imeelezwa kuwa watu walikuwa na hofu ya kupita katika msitu huo kwa hofu ya kudhurika. Watu walilazimika kupiga hodi wakati wanapotaka kupita sehemu hiyo. Msanii anatusimulia hivi:

> "Mzimu wa Watu wa Kale ni kichaka kinachosumbua watu wa sasa. Wale wanaojua vitisho vya mizimu, hawaipiti ovyo ovyo njia hiyo bali huchagua nyakati za kupita. Watakwambia kuwa Adhuhuri na Magharibi usipite mahali hapo, maana wakati huo mizimu wanasali. Na pindi ukipita wakati mwengine, basi lazima juu yako kupiga hodi, na ukisahau kupiga hodi, basi litakalokupata usilie na mtu- labda ulie na mizimu tu(uk. 16)."

Dondoo hii inaonesha mwandishi anavyokisawiri kichaka chenye kutisha kutokana na kudhihiri mambo yasiyo ya kawaida katika kichaka hicho jambo linalosababisha kuibua hofu. Katika jamii nyingi za Afrika hadi sasa zipo sehemu ambazo huaminika kuwa na nguvu za kiza na hivyo mizimu huaminika kuwa ina nguvu kuliko binadamu katika maeneo hayo. Kwa mfano, katika jamii ya Wapemba yapo maeneo ambayo hutambulika kama "panga" ambapo maeneo hayo ni makaazi ya majini. Katika maeneo hayo watu huenda kufanya matambiko na hata kutupa vyakula (chano) kama sehemu ya sadaka ya majini ili kufanikisha mahitaji yao.

Kupitia nadharia ya uhalisiajabu chini ya muhimili wake unaoeleza kuwa: Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Mtafiti amebaini kuwa mandhari ya kichaka cha Mzimu wa Watu wa Kale ni mandhari ya uhalisiaajabu kwa vile imekiuka uhalisia.

4.4.2.2 Mandhari ya Ndani ya Mzimu

Ndani ya Mzimu wa Watu wa Kale ni mandhari nyengine iliyosawiriwa kiuhalisiajabu. Ndani ya msitu huo msanii ameeleza kwamba Bwana Msa alikutana na mazingira yanayotisha na ya kuogopesha. Mathalani, msanii anaeleza kuwa Bwana Msa alipochungulia ndani alibaini kwamba kulikuwa na kiza kama uwanda wa Akhera. Pia, ilisikika sauti moja kubwa kama maporomoko ya maji. Msanii anasimulia kwa kusema:

> “Bwana Msa alichungulia tena. Ndani mulikuwa na kiza kama uwanda wa Akhera, kiza kilikuwa kimetapakaa, kinavuja! Sauti za komba na mabundi- wasiojua, kwa sababu ya kiza kilichozagaa, kama kumekwisha kucha- zilihinikiza sauti zote za vidudu zinazosikilikana kichakani au mashamba wakati wa usiku. Lakini juu ya sauti zote hizo, ilipaa sauti moja tu kubwa kuliko zote iliyokuwa ikiendelea bila ya kusita na ikivuma kama maporomoko ya maji. Bwana Msa alishindwa kuelekeza sauti ile ni ya nani, na ndiyo iliyomrudisha uso wake nyuma alipojaribu kuchungulia ndani. Kwa kiasi tu, alielekeza kuwa ni sauti ama ya gurudumu, kama gurudumu la motokaa, linazunguka na kwenda mbio humo ndani ya mzimu, au mkokoto wa kitu kirefu kizito kama chatu, kinajikokota kwa upesi juu ya majani makavu. Lakini mara ilimjia hisi kwamba kila dakika sauti ile ilizidi kuwa kubwa kwa sababu ilikuwa ikisogea mbio mbio kukaribia, ‘mlangoni,’pale walipo wao. Nani anaendesha gari ndani ya mzimu? Tuseme wale maiti?
>
> …. Bwana Msa alikitoa kichwa chake, akampisha mwenziwe, na huku akimwambia “Hebu sikiliza, Najum. Mna sauti ndani kama mna watu wanaendesha gari, tena linakuja kuku huku tuliko; je unalisikia?”
>
> Najum akatia kichwa chake kusikiliza, na hukuakisema, “Labda mizi-’’ (uk 22- 23).

Dondoo hili linaonesha namna mandhari ya Mzimu wa watu wa kale yalivyokuwa na maajabu. Sauti zinazoelezwa na mhusika Bwana Msa zinakiuka uhalisia wa mandhari ya uhalisia zilizozoeleka katika jamii. Ni katika misitu ya kawaida huwa

hakusikiki mivumo kama ya vyombo vya moto walivyovisikia Bwana Msa na Najim. Katika mazingira ya uhalisia, msituni inatarajiwa kusikika milio ya wanyama na ndege ambao wamekuwa wakiishi katika misitu hiyo.

4.4.2.3 Mandhari ya Sebule

Mandhari nyengine ya uhalisiajabu iliyojitokeza katika riwaya hii ni sebule ya mzimuni. Katika sebule hiyo msanii anaeleza kuwa kulikuwa hakuna mijiti lakini kulikuwa na makaburi saba ambayo yalikuwa yamenakishiwa na kupambwa kwa mapambo ya Kichina. Makaburi hayo yalikuwa yakivutia. Msanii alisimulia mazingira haya kwa kusema:

> Waliendelea kimya kimya kwa kitambo kidogo. Sasa wamefika katikati ya mzimu, na hapo hapakuwa na miti kabisa isipokuwa ile ya pembezoni iliyofanya au kujenga kuta zake za nje. Hapo palikuwa wazi, na jua liliingia kwa nguvu. Ardhi yake ilikuwa kama jangwa la Sahara, mchanga mkavu mtupu uliokwenda dhiraa nzima chini.
>
> Baada ya kimya kirefu kilichopita. Bwana Msa akaanza kusema, “Nadhani hii ndiyo ile sebule ya mzimu. Tazama kule! Yale ndio makaburi ya hao watu wa kale. Yatazame namna yalivyo marefu na jinsi yalivyopendeza!”
>
> Najum alitazama. Kwa kule, inapata hatua mia kulikuwa na makaburi marefu saba, yanapata futi kumi na tano kila moja, nayo yamepangiliwa kwa sahani na vibakuli vya sini, na pembenipembeni mmepachikwapachikwa bendera; yamejengwa kwa chokaa ya asili, ngumu kuliko saruji, yanang’aa juani (uk. 34).

BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa sebule ni chumba maalumu cha nje kilichoelekezwa na baraza au upenu wa nyumba hiyo kinachotumika kuzungumzia au kupokelea wageni. Kupitia dondoo hii inaonyesha kuwa sebule ya mzimuni ni sehemu iliyo wazi ambayo iko katikati ya mzimu ikiwa na mchanga mkavu usioruhusu miti kuota, pembezoni mwa sehemu hiyo kumezungukwa na miti mithili

ya ukuta. Mandhari hii ni ya uhalisiajabu kwa vile si uhalisia kuota miti na vichaka na kubaki sehemu maalumu, ndogo, iliyowazi bila ya miti, huku ikizungukwa na ukuta wa miti ulioshikana kama kwamba umetengenezwa na mwanadamu kwa kukusudia. Pia, namna makaburi yalivyo marefu na mapambo yaliomo mtafiti ameona uhalisiajabu ambao umekiuka uhalisia wa hali ilivyo katika maisha ya kawaida.

4.4.2.4 Mandhari ya Makaburini

Mandhari ya makaburini yaliomo ndani ya mzimu wa watu wa kale ni mandhari nyengine inayotuibulia uhalisiajabu. Msanii kupitia riwaya hii alisema kwamba mara baada ya Bwana Msa kuyapita makaburi mchanga ulikuwa kidogo na kutokea jangwa. Pia, kulikuwa na kijito cha maji lakini kijito hicho hakikuwa na maji isipokuwa unyevunyevu. Msanii anasimulia hivi:

> Kuyapa makaburi kisogo tu, mara mchanga ulisita kuwa mwingi, na jangwa likageuka uwanda. Kwa mbele kidogo, kilipita kijito cha maji- si kijito kitu, la vimajimaji na unyevu unyevu tu katika ardhi (uk. 37).

Kupitia dondoo hili mtafiti amebaini kwamba, mazingira ya mzimuni yaliibua matukio mbalimbali ya kiajabuajabu yenye kutisha na kushangaza. Kama vile kitendo cha kusita mchanga kuwa mwingi, jangwa kugeuka uwanda, na kuibuka kwa kijito cha maji ghafla. Matukio hayo yasingeweza kutokea katika hali ya kawaida kwani sehemu ya makaburi ni jangwa na pindi ukisogea mbele kidogo unakuta sehemu yenye rutuba na maji kwa ajili ya kilimo.

Vile vile, katika makaburi hayo mtafiti amebaini kuibuka kwa uhalisiajabu. imeelezwa kuwa Bwana Msa waliikuta maiti ya bwana Ali imeroa damu. Pia, maiti

ya Bwana Ali ilikuwa imepakata boga lakini haikua na kichwa. Tukio hili lilidhaniwa na Bwana Msa kwamba ulikuwa ni mchezo mmoja wa vile vizuu vinavyopatikana katika mzimu wa watu wa kale. Msanii alisimulia kwa kusema kama ifuatavyo:

> “Ndiye kweli bwana Ali, lakini hana kichwa. Koti lake la kaki lilikuwa limeroa damu. Miguu yake kainyoosha mbele yake na juu ya mapaja yake alikuwa amepakata boga tu wala si kichwa chake, kama ilivyoonekana kwa mbali. Nadhani ulikuwa mchezo mmoja wapo wa vile vizuu vya watu wa kale, au makima wa kule kichakani kumpakatisha boga maiti yule. Kwa kweli, yalikuwa mandhari mabaya sana, ya kusisimisha mwili” (uk 36).

Kupitia nukuu hii mwandishi amechora mandhari iliyokuwepo maiti ya Bwana Ali kuwa ni ya ajabu. Hii ni kutokana na kuwa alikutwa tayari amekufa na kupakatishwa boga badala ya kichwa chake. Kitendo hiki si cha kawaida. Ilitarajiwa kuwa wauaji wangalifukia maiti ya bwana Ali ili kupoteza ushahidi badala ya kuihusisha mizimu kama ni watendaji wa tukio hilo.

Kwa kurejelea nadharia ya uhalisiajabu mtafiti amebaini kuwa mandhari yanayosawiriwa katika mzimu wa watu wa kale yanaoana na nadharia ya Uhalisiajabu. Kama wasemavyo Njogu na Wafula (2007)kwamba katika kazi za uhalisiajabu wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Hivyo basi, msanii anaweza kusema kuwa mandhari haya yametumika na msanii kwa makusudi ili kuikiusha riwaya hii na mandhari za kihalisia.

Salim (2015)anafafanua kuwa waandishi hutumia mandhari ya kidhahania ikiwemo ya mandhari ya uhalisajabu ili kukwepa mkono mrefu wa dola wakati wa kufichua

maovu yaliyokithiri katika jamii. Kwa mfano Robert ingemuwiya vigumu kuichapisha kazi yake ya riwaya ya *Kusadikika* kwa matumizi ya mandhari halisi kutokana na vikwazo vya dola ya kikoloni iliyokuwepo Tanganyika wakati huo.

4.4.3 Uzungumzinafsi

Hii ni mbinu ambayo mhusika huzungumza na nafsi yake mwenyewe. Wamitila (2008) anaifafanua mbinu hii kuwa ni mtindo wa kuyadhihirisha mawazo ya mhusika kwa njia ya kujizungumzia. Pia uzungumzinafsi uko wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja. Aidha Homo (2015) anaeleza kuwa uzungumzinafsi unahusu monolojia, yaani muhusika anajizungumzia pekee yake. Kutokana na kujizungumzia huko wasimuliwaji huweza kupata fursa ya kufahamu kile kinachoendelea katika akili ya muhusika ambapo wasimuliwaji huweza kubaini sifa au tabia za muhusika huyo pamoja na maudhui yanayoibuliwa.

Data zilizokusanywa kutoka katika riwaya teule zimebainisha kwamba mbinu ya uzungumzinafsi imetumiwa na msanii kama sehemu ya mtindo wa uhalisiajabu. Mbinu hii imetumiwa na mhusika Bwana Msa wakati anapojiuliza kuhusu karatasi aliyoiokota ambayo ilikuwa ni stakabadhi ya kuuziana shamba. Ajabu ni kwamba karatasi hiyo haikuwa na tarehe wala saini. Msanii anasema hivi:

> Bwana Msa aliuliza, “Mtu akikaa akichorachora upuuzi tu, atachora kitu cha maana au cha upuuzi tu vile vile?” Lakini sauti alivyokuwa akisema bila ya kumtupia jicho sahibu yake, alionyesha kuwa anasema na nafsi yake tu kwa sauti (uk. 30).

Katika dondoo hii mwandishi anaonesha kuwa Bwana Msa alikuwa akipingana na nafsi yake kuhusu stakabadhi iliyoandikwa na Bwana Ali kuwa ilikuwa na maana au ni upuuzi tu. Huu ni uhalisiajabu kwa vile mtu hawezi kuchora au kuandika kitu cha

maana na chenye umuhimu bila ya kuwa na dhamira fulani. Pia, mtu hawezi kuandika waraka wa manunuzi bila ya kuwa na tarehe na saini.

Mbinu hii ya uzungumzinafsi kama sehemu ya uhalisiajabu ilijitokeza kupitia mhusika Najim. Najim alikuwa akijisemea kuhusu stakabadhi ile ambayo haikuwa na saini wala tarehe. Najim aliamini kuwa stakabadhi ile ilikuwa ni upuuzi tu. Msanii ameeleza kuhusu suala hili pale aliposema:

> Najum alitazama akaona sasa Bwana Msa anasema maneno ya upuuzi; maana mambo mawili haya aliyoyataja yanapingana yenyewe kwa yenyewe na yanarejea kule kule kuwa karatasi ile ni upuuzi. Ikiwa ile ni stakabadhi hakika, basi yule Banyani alikuwa mpumbavu asiipokee kwa Bwana Ali akawa nayo mwenyewe. Na vile vile ilivyokuwa stakabadhi yenyewe haina sahihi wala tarehe, basi inafuta yale masala hakika yake, na kuifanya stakabadhi ile vile vile ni upuuzi tu. Kinyume cha mambo, leo, inaonyesha dhahiri kuwa Bwana Msa ana wazimu! (uk. 31)

Kupitia nukuu hii mwandishi anaonyesha kuwa jambo hilo haliwezekani kuandika stakabadhi bila ya kuwa na saini wala tarehe. Katika hali hiyo Najum alijiuliza maswali mbali mbali yanayohusiana na maandishi hayo. Jambo hili lilimfanya Najum ayaone mambo hayo ni kinyume cha mambo. Aidha Najum alimwona na Bwana Msa hayuko sawa wakati ule.

Mbinu hii ya uzungumzi nafsi kama sehemu ya matumizi ya mbinu ya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* inajitokeza wakati Najim alipoiona maiti ya bwana Ali. Msanii alieleza kuwa Najim alipatwa na mshituko baada ya kuiona maiti ya bwana Ali imepakata kichwa chake. Kwa tukio hili aliona kuwa bwana Ali amefanya jambo la kujitakia kutokana na kwamba anajua msitu huo ni mbaya. Tunaelezwa kuhusu tukio hili msanii anaposema:

> Najum akazidiwa na hofu. Kumbe yule aliyekuwa amekaa pale chini ya kaburi hali amenyoosha miguu yake na kupakata kichwa chake, alikuwa Bwana Ali! “Nini kilichompeleka mzimuni magharibi, wakati watu wanakatazwa kupita, na kukaa chini ya mzimu kama kwamba yuko kwake! Ikiwa habari zisemwazo za mizimu ni kweli, (na kwa namna hii zinaonyesha kuwa ni kweli) basi yaliyompata Bwana Ali ni stahili yake, maana alijuwa kuwa wakati wa magharibi hakuna ruhusa ya kupita, naye alikwenda kusudi kughasi. Lakini alitaraji nini?” (uk. 35-36).

Kutokana na maelezo haya mtafiti amegundua kuwa kipengele cha uzungumzinafsi kimetumika ili kuonyesha maajabu ya kichaka cha Mzimu wa watu wa kale. Kichaka hicho kiliogopewa na watu. Pia, inaonesha kuwa wale waliopata matatizo katika kichaka hicho walionekana wameikasirisha mizimu na kwa sababu hiyo walilaumiwa wenyewe.

Aidha, kipengele chengine cha uzungumzinafsi unajitokeza pale Spekta Seif alipokuwa akisema na kujiuliza nafsi yake kuhusu kifo cha Bwana Ali ambapo alishangazwa kwa kuona kichwa mbali na kiwiliwili mbali. Tukio hili linasimuliwa na msanii hivi:

> Njiani, walikuwa wakienda kimya ila yeye peke yake alikuwa akipita akisema polepole kama anasema peke yake. “Nani hasa aliyemwua Bwana Ali? Ilikuwaje hata kichwa kikawa mbali na kiwiliwili mbali? .....” (uk. 51).

Dondoo hili linaonesha namna usimulizi huu unavyoibuwa tukio la maajabu. Maajabu haya ni yale ya mauaji na hatimae kuchukua mwili na kuacha kichwa. Pia, tukio hili linaonesha maajabu kwamba vyombo vya dola havijui kinachoendela kuhusiana na tukio hili lakini Bwana Msa anabaini kile kilichokuwa kikiendelea.

Katika sehemu nyengine Spekta Seif anatumia mbinu ya uzungumzi nafsi kama sehemu ya uhalisiajabu. Mbinu hii ilitumika pale Spekta Seif anapojiuliza maswali

mbalimbali wakati akifikiri kuhusu mauaji ya Bwana Ali. Mtunzi anasimulia tukio hili hivi:

> Akasimama kuitazama maiti mara ya mwisho, “Tazama shingo ilivyo safi. Lazima aliyeua alikuwa na nguvu nyingi, maana hapana ila dharuba moja tu aliyompiga, akakirusha kichwa; mambo gani haya? Inaonyesha kuwa ni mtu mmoja tu aliyeua. Aidha, yaonyesha kuwa hakuwa peke yake katika kazi hii. Wenziwe gani hao? Na kwa nini akaweka boga mapajani mwake? Lo, mambo haya yataharibu akili za watu wote waliopo hapa Baraste, na itikadi ya Mzimu wa Watu wa Kale itazidi kuwa na nguvu” (uk. 54).

Katika dondoo hili msanii anaonesha namna mzimu wa watu wa kale ulivyokuwa ukiwaogopesha watu. Kutokana na woga huo ni dhahiri kwamba kifo cha bwana Ali kitazidisha watu waendelee kujenga hofu kwa mzimu wa watu wa kale. Kitendo cha watu kuogopa msitu kwa namna inavyosimuliwa katika sehemu hii kimevuuka uhalisi na badala yake kimekuwa cha maajabu.

Moja ya msingi wa nadharia ya uhalisiajabu ni kuwa uhalisiajabu unapinga uhusiano na kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbali mbali kama vile uhalisi wa ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana. Hivyo basi, kupitia mhimili huu wa uhalisiajabu mtafiti amegundua matukio aliyoyaeleza katika sehemu hii yanalandana na nadharia ya Uhalisiajabu. Kwa mfano, ukale wa stakabadhi zilizokuwa zikiandikwa kwa miongo kadhaa umeingiliwa na usasa. Pia, suala zima la matumizi ya misitu, mito, majabali ni vipengele muhimu katika fasihi za mrengo wa uhalisiajabu.

4.4.4 Matukio ya Kiuhalisiajabu

Matukio ni mtiririko wa visa au mawazo katika kazi ya fasihi. Olali (2010) anaeleza kuwa katika uhalisiajabu matukio huwa ya kifantansia au ya kiajabujabu au ya

kichawi kwa namna ya moja kwa moja. Aidha, kutokea kwake huonekana kama ya kawaida tu. Mara nyingi matukio yake huwa ni changamano yanayoonyesha urejeshi. Mbali na hayo, tanzu za fasihi simulizi huweza kutumika. Wamitila (2008)anafafanua kuwa riwaya zinazofuata mtindo wa uhalisiajabu huwa na matukio ambayo ni vigumu kuyaeleza katika uhalisi.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* data zinaonesha kuwa kuna matukio ambayo yanaibua uhalisiajabu. Moja kati ya tukio la uhalisiajabu ni lile linalohusu ugonjwa wa Kipwerere. Inaelezwa kuwa huenda Kipwerere alirogwa na wachumba waliokuwa wakimchumbia ama alikumbwa na shetani wakati akipita katika msitu huku akiwa anakula ndizi. Mwandishi anasimulia tukio hili hivi:

> Mambo yalipokithiri, wazee wake walifika kwa waganga kutazamia, nao kila mmoja alisema lake. Wengine walisema kuwa amerogwa na wachumba waliokuwa wakimtaka wakamkosa. Wengine walisema kuwa amedhuriwa katika kile kichaka kiitwacho 'Mzimu wa Watu wa Kale', alipokuwa akipita siku hizo bado kigori na huku anakula ndizi ya kipukusa; kwa hiyo, shetani wa mzimuni alimshika na kumpanda kichwani wala hatamtuliza na kumpa nafasi ila apate chano cha ng'ombe. Wazee wa Kipwerere walipendekezewa na aguo la pili kuwa mtoto wao kasibika na shetani, maana waliona inamkinika kuliko lile aguo la kwanza lililoagua marogo ya mchumba waliomkosa, kwani hakutokea hata mmoja katika hao waliootea uchumba, kwenda kumposa- kabla ya Bwana Ali - akakataliwa.
>
> Na kwa hiyo kila dhofu lihali ikizidi kumkondesha Kipwerere wazee wake humshika mumewe Bwana Ali atowe ng'ombe mmoja ili apewe chano mtoto wao apate kupumzika; lakini Bwana Ali huzidi kuwapa ahadi za mbele tu, mwaka baada ya mwaka, mpaka leo hii (uk. 8-9).

Katika dondoo hili msanii ameonesha namna viumbe wanavyopewa nguvu za kimiujiza za kumpa mtu magonjwa. Matokeo haya hayajitokezi katika kazi za kihalisia. Ingawa kwa ukweli katika jamii nyingi za Afrika imani kama hizi zipo na

zinaendelea kutiiwa na baadhi ya wanajamii. Kutokana na ukweli huu ndio maana waganga wa kienyeji wamekuwa wakipewa nafasi ya kuwa waaguzi wa mambo ambayo hayawezi kuthibitika kwa kutumia misingi ya sayansi.

Matukio kama haya yanawiyana na nadharia ya Uhalisiajabu. Kama asemavyo Wamitila (2013) kwamba kazi za kihalisiajabu huwa na matukio ambayo huchukuliwa kama matukio ya kawaida katika ulimwengu wa kiuhalisia. Matukio hayo huwa yamedenguliwa. Kwa mantiki hiyo huwa yamekiuka misngi ya kazi za uhalisia.

> Kwamba wewe unadhani- kama wanavyodhani watu wengine- kwamba mtu akichagawa hujiwa na shetani au hupandwa na pepo aliyetoka bahari ya saba au ardhi ya saba, yaani yule binadamu kwa wakati ule huwa kama 'kiti' chake. Vyema, lakini 'kiti cha shetani ni bianadamu, na binadamu ana sehemu mbili, kiwiliwili na roho, sasa, mtu akichagawa, shetani hukaa wapi hasa, mwilini au rohoni mwake? (uk. 12).

Aidha, tukio jengine la uhalisiajabu linajitokeza wakati mwandishi anaposimulia mapisi ya watu wa mapangoni. Imeelezwa kwamba watu wa mapangoni walichukua panga, wakaijaza maji ambayo yalikuwa yanaeleweka na waganga tu. Huku wakiwa na manuizo na papo hapo pakatokea moshi mkubwa na mara moshi ule ulipokwisha watu wa mapangoni walikuwa tayari kuagua na walisema kuwa watu wale saba walitoka katika bara la Waajemi. Kisa hiki kinasimuliwa hivi:

> Watu wa mapangoni walichukua kombe ya chaza anayeitwa Panga, wakaijaza maji yao ya siri yanayojulikana kwa waganga tu kuwa ni 'Maji ya Mkondo wa Mauya;' wakasema wakiomboleza maneno yasiyofahamika; kisha wakayamwaga maji yale katika jiwe la marjani, na hapo hapo ukatoka moshi mwingi. Moshi ule ulipokwisha, watu wa mapangoni walikuwa tayari kuagua. Walisema kuwa watu wale saba wametoka katika bara la Waajemi, katika mji wa Al Hasa; wametoka watokako wakipita kuitafuta Akhera iliko; na walipofika Jongomeo, Mwenyezi Mungu akawateremshia mauti; roho zao zikahama miilini mwao. Lakini kweli hasa kwa mwenye kutambua (uk 16-17).

Katika dondoo hili mtafiti ameona namna masimulizi haya yalivyo na sifa ya kisasili ambapo tukio hili limesawirwa kihalisiajabu. Masimulizi ya matukio kama haya kwa kawaida yanayaonanekana katika ngano za fasihi simulizi ambazo nazo huwa zinasawiriwa kwa matukio ya uhalisiajabu. Pia, tunayosimuliwa katika tukio hili yamechota sifa za usihiri sifa ambayo ni moja kati ya sifa ya uhalisiajabu.

Tukio jengne la uhalisiajabu ni lile linalomhusu Bi Kazija, mama yake Kipwerere. Katika tukio hili msanii anaeleza kuwa Bi Kazija alikuwa na uwezo wa kufahamu maneno ya shetani. Kutokana na uwezo huo aliweza kubani kwamba kulikuwa na jambo baya linakuja. Kafara ya kuondokana na janga hilo ni kuchinja mbuzi mwekundu. Tunasimuliwa tukio hili hivi:

> Kwa wakati ule Ahmed alirudi kwa wenziwe akawaeleza kuwa Bi Kazija, mama yake Kipwerere, anafahamu maneno ya shetani wa mwanawe, na kaagua kuwa kuna jambo baya mbele yao linakuja jambo kama la kifo-na kafara lake linataka mbuzi mwekundu achinjwe ‘waruke damu’. Lakini alipotoka pepo kichwani, Kipwerere kashikilia lazima aende mtu Baraste kumsikiliza mumewe, na kama hapana mtu wa kwenda, basi atatoka yeye mwenyewe aende, maana wakati ule ulikuwa unapata saa mbili naye hajarudi bado (uk.13).

Matukio haya yaliyojadiliwa katika sehemu hii yanalandana na nadharia ya Uhalisiajabu. Kama asemavyo Wamitila (2013)kwamba uhalisiajabu umefungamana na sanaajadi kama vile visasili. Visa vinavyoelezwa katika sehemu hii ni mfano wa visasili ambavyo huwa vinatambwa katika jamii za Afrika. Katika baadhi ya jamii za Afrika wahusika waganga wa kienyeji huwa na nguvu za kisihiri kama tunavyoona katika tukio hili. Pia, suala la uganga wa jadi ni jadi ya bara la Afrika.

4.4.5 Usimulizi wa Kiuhalisiajabu

Masimulizi ni mbinu ambayo mtunzi huitumia kumwelezea muhusika juu ya matendo yake, mienendo na tabia zake. Katika kazi za fasihi waandishi wana fursa ya kujijengea usimulizi wa tarjiba na maarifa yao bila ya kubanwa. Mwandishi ana uwezo wa kiuungu wa kupenya katika fikra za wahusika wake kwa kubainisha maarifa zaidi ya yale ambayo wahusika wake wanayafahamu au kuyasimulia. Aidha mwandishi anaweza kuwapa wahusika wake maarifa zaidi ya yale ambayo wahusika wake wanayafahamu au kuyasimulia (Genette, 1972).

Vile vile, Wamitila (2013)anadai kuwa msingi mkuu wa riwaya ya uhalisiajabu ni kuwepo kwa sifa ya ukiushi kwa kiwango kikubwa katika muktadha wa usimulizi. Naye Genette (ameshatajwa) anafafanua kuwa katika kipengele cha usimulizi katika kazi za uhalisiajabu, mwandishi anaweza kutumia mbinu ya uhalisiafifi ambapo huweza kuyaumba matukio katika hali ya kindoto au kisaikolojia yanayotokea katika ung'amuzibwete.

Hivyo basi usimulizi wa uhalisiajabu katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale umejitokeza wakati msanii anaposimulia namna Bi Kazija alivyogundua kuwa kulikuwa na hatari imemkabili Bwana Ali. Linaelezwa tuko hili pale msanii anaposema:

> "Yule bibi hapana shaka, alikuwa, na wasiwasi tangu hapo. Wakati mwingi huambiwa, 'roho ni bao' yaani huona yatakayo kuja kabla hayajatokea. Maneno haya, mara nyingi huwa ni kweli, roho yake yule bibi iliruka kwenda kutazama matokeo ya siku ile, na ilivyokuwa mumewe mpaka sasa hivi hayuko nyumbani kama desturi yake, roho yake yule bibi ilianza kuagua mambo iliyoyaona katika ukaguzi wake. Roho ilistuka ilipoona 'kiza,' 'hapana' yaani 'kiza kitupu'; na, kwa kweli, kiza kitupu hapana ila mauti." Roho ilizidi kutegua ilipoona kitu 'safi kabisa,' tena 'chekundu.' Kitu gani hicho kilichokuwa safi

> kabisa tena chekundu isipokuwa damu? Yaani, kwa ufupi, yule shetani, au roho ya yule bibi, ameagua kuwa Bwana Ali ameuwawa-" (uk. 12)

Katika dondoo hili mtafiti amebaini uelewa wa mambo usiokuwa wa kawaida wa Bi. Kazija. Huu ni mfano wa ung`amuzibwete binafsi ambao huangukia kuwa ni moja ya sifa ya kazi za uhalisiajabu kama inavyoonekana hapo juu ambapo Genette (1972)ambapo anasema kwamba katika kazi za kihalisiajabu mwandishi ana uwezo wa kiungu wa kupenya katika fikra za wahusika wake kwa kubainisha maarifa zaidi ya yale ambayo wahusika wake wanayafahamu au kuyasimulia. Aidha mwandishi anaweza kuwapa wahusika wake maarifa zaidi ya yale ambayo wahusika wake wanayafahamu au kuyasimulia.

4.4.6 Umahuluti wa Kiutamaduni na Kitanzu na Mwingilianomatini

Herman na wenzake (2005)wanaeleza kuwa riwaya ya kiuhalisiajabu inahusishwa na mwingiliano wa sifa za kiutamaduni za jamii na maeneo mbalimbali. Sifa za kimahaluti wa kitamaduni zinapatikana katika fasihi kwa mapana sana. Kipengele hiki kimechukuliwa na baadhi ya wataalamu kama mojawapo ya kipengele kinachowavutia waandishi wengi wanaoandikia muktadha wa baaada ya ukoloni kuupendelea mkabala huu kama bunilizi zao.

Mbinu hii kama sehemu ya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imetumika wakati msanii akisimulia tukio la Bwana Msa alipokwenda kwenye Mzimu wa watu wa kale. Imeelezwa kwamba Bwana Msa alipiga hodi mara tatu kama sehemu ya utamaduni wa watu wa hapo. Tukio hili linasimuliwa hivi:

> "… Bwana Msa alitangulia, akapiga magoti akasema "Hodi" mara tatu, kisha akatia uso wake ndani kuchungulia. Kuna vile Najim alistaajabu si haba. Bwana Msa aliyekuwa akisubu mambo ya mizimu kwa maneno ya bezo namna ile imemjia kuutukuza mzimu namna hii? Najim hakuweza kusubiri, bali aliuliza kama anachokoza, "Unapiga 'hodi' kwani unaamini nini kitendawili chao cha mizimu?" (uk. 27)

Katika dondoo hili msanii anaonesha namna Bwana Msa anavyopiga hodi katika msitu huo kama ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Hata hivyo Najim anashangazwa na tukio hilo na kuona kuwa kufanya hivyo ni fumbo kama lile la kitendawili. Mawazo ambayo yanaonesha kwamba Najim haamini utamaduni huo.

Pia, mbinu hii ya muingiliano wa kiutamaduni na kitanzu umetumiwa na msanii wakati akisawiri wahusika Bwana Msa na Najim. Bwana Msa anamueleza Najim kwamba iwapo amemstua itakuwa amemroga. Hii ni imani ya kitamaduni ambayo katika jamii ya Uswahilini huchukuliwa kama utamaduni wa Mswahili. Linaelezwa tukio hili kama ifuatavyo:

> "Ahlan, Najum! Nimekustua au nimekuzindua? Ikiwa nimekustua, itakuwa nimekuroga; lakini, ikiwa nimekuzindua itakuwa nimekuzindua. Bali ilivyokuwa hapo ulipochutama pana zindiko langu, na litayari kumzingia mtu yoyote atakaye jitia umbea, hapana shaka kwamba kutokea kwangu hivi sasa nikasimama mbele yako namna hii, kumekuzingua" (uk. 4).

Tukio jengine ambalo limesimuliwa kihalisiajabu kama sehemu ya umahuluti wa utamaduni unajitokeza kwa Mama Kipwerere. Msanii anaeleza kuwa Mama Kipwerere baada ya kubaini ugonjwa alionao mtoto wake, aligundua kuwa ugonjwa ule ulikuwa unatokana na shetani. Msanii anasimulia tukio hili hivi:

> Mama Kipwerere alipoona hali ya mwanawe namna ile, alifahamu kwa upesi kuwa ugonjwa ule wote unatokana na yule shetani anayekwambwa naye na kwa hiyo alijaribu kumpumbaza mwanawe na kumletea shauri la ‘kumshika sikio’ shetani huenda akampa nafasi kidogo. Kipwerere, alivyokuwa na yeye yumo katika itikadi zile, na vile vile hawezi kuvunja shauri la mzee wake, aliridhi kufanyiwa yale, ndipo bikizee akachukua kitezo, akaenda uani na jikoni kutafuta moto (uk. 9).

Dondoo hili linaonesha namna suala la utamaduni wa Waafrika linavyojidhihirisha. Katika jamii za Afrika Tanzania ikiwemo wapo watu ambao wamekuwa wakiamini uwezo wa shetani na hivyo kuamini kuwa mashetani wamekuwa na uwezo wa kusababisha magonjwa mbalimbali kwa wanadamu. Ili kuondokana na shetani huyo ndio maana Bi. Kizija anatumia kitezo ili kumtaka shetani asilete madhara hayo.

Sehemu hii imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Vipengele vilivyobainishwa ni pamoja na wahusika wa kihalisiajabu, mandhari za uhalisiajabu, uzungumzi nafsi, matukio ya kihalisiajabu, umahuluti wa kitamaduni, kitanzu na Mwingiliano matini. Kufanya hivyo mtafiti aliweza kujibu swali la kwanza la utafiti huu. Hivyo basi, katika sehemu ifuatayo mtafiti amefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data zinazohusu namna vipengele vya uhalisiajabu vinavyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

4.5 Dhamira Zilizobainishwa kwenye Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya Teule

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lililenga kutafiti namna vipengele vya uhalisiajabu vinavyoibua dhamira katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Data zilizokusanywa na mtafiti zilionesha kuwa vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya

ya *Mzimu wa Watu wa Kale* vinaibua dhamira kadhaa zinazoihusu jamii. Hivyo katika sehemu hii mtafiti amefanya uchambuzi na uwasilishaji wa namna vipengele vya uhalisiajabu vinavyoibua dhamira katika riwaya teule.

4.5.1 Imani za Jadi

Data zilizokusanywa katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* zinaonesha kuwa mwandishi ametumia wahusika wa uhalisiajabu kuibua dhamira ya imani za jadi. Kama mtafiti alivyoeleza hapo kabla kwamba msanii amemchora mhusika Kipwerere akiwa ni mhusika anayeibua maajabu. Kipwerere anapatwa na matatizo lakini hajali kwa ile kinachomtokea. Kwa mfano anapopata ajali na kujeruhiwa vibaya hajali. Mtunzi anasimulia hivi:

> Baada ya muda kitambo muwele, alianza kuharakisha kichwa chake kidogo kidogo, na baadae akaanza kutika na kuzungumsha kichwa huku na huku, mpaka kikashika kasi-shetani tayari kichwani. Kipwerere alizuka pale alipokaa akamsukuma mama yake chini, yeye akajitupa chini kwa nguvu sana, kichwa chake kikafika juu ya ncha ya ukingo wa baraza, akapiga siyahi ya nguvu sana kisha akainuka hali damu zinamtoka kichwani…Kipwerere, taratibu kama siye, aliondoka pale chini, damu zinamchiririka usoni kama mfereji, akarudia msalani kwake, akakaa tena kama alivyokuwa kwanza, amenyoosha miguu upande wa kibla na kumuashiria mama yake ambaye sasa hivi amekwisha jizoazoa pale chini aliposukumwa, aje kumfunika tena (uk.11).

Katika dondoo hili mtafiti anaonesha namna mhusika Kipwerere anavyosawiriwa akifanya matendo ya kiajabuajabu yenye kukiuka uhalisia. Matendo kama haya yamekuwa yakifanywa na baadhi ya wanajamii wa Afrika. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba baadhi ya Wazanzibar wamekuwa na imani kama hizi. Hata pale wanapokumbwa na matatizo baadhi yao huamini kwamba ni urogi unaotokana na mashetani.

Pia, katika kuelezea dhamira hii ya imani za kijadi msanii alitumia mhusika shetani. Shetani anasawiriwa kiuhalisiajabu. Msanii anaonesha namna jamii inavyoamini kuwa shetani ana nguvu na uwezo wa kuingia katika mwili wa binadamu na kumfanya awe hajitambui. Kutokana na hali hiyo mtu aliyekumbwa na shetani huweza kufanya matendo ambayo si ya kawaida katika maisha ya binadamu. Msanii anasimulia kwa kuesema:

> "…Alipokwisha funikwa, shetani alianza kutika na kuzungumsha kichwa kwa nguvu sana, kisha akasema, "Nimeona! Nimeona! Kiza! A-aaa! Hapana kitu! Safi kabisa! Hapana kitu! Nyekundu –u! ..." (uk.11)

Dondoo hili linaonesha namna Kipwerere anavyoongozwa na Shetani ili kuagua matukio yaliyompata Bw. Ali. Mawazo kama haya ni ya jadi katika jamii za Afrika. Hali hii imekuwa kama sehemu ya ujumi wa Waafrika. Kutokana na ukweli huu ndio maana katika tenzi za kale kama vile Utendi wa Fumo Liyongo umetumia mhusika Fumo Liyongo ambaye ana nguvu za usihiri katika kitovu chake. Ndio maana Fumo Liyongo hadhuriki isipokuwa kwa kumchoma sindano ya shaba kitovuni mwake.

Pia, dhamira ya imani za kijadi imejadiliwa kupitia mhusika mama Kipwerere. Mhusika huyu amechorwa akiwa ni mganga wa kienyeji. Katika kuisawiri dhamira ya imani za jadi msanii anaeleza kuwa:

> Aliingia ndani chumbani akampa habari mwanawe kuwa sasa ni kushikwa sikio. Kipwerere alijizoazoa pale kitandani alilipolala akatangulia uani; mama mtu alifungua kisanduku akatoa kanga mbili za kwenda kumfunika muwele. Alimkuta muwele amekwisha kukaa juu ya mswala na miguu yake ameinyoosha upande wa kibla. Mama Kipwerere alimfunika mwanawe kanga zote mbili gubigubi, tangu kichwani mpaka nyayoni, naye akarudi na kazi yake ya kutengeneza moto na manukato ya kumfukizia. Katika kifurushi kilichokuwa karibu yake alitowa pachori na pakanga, udi na ubani wa makaburini, kusti na mea, alipokwisha vitia vyote hivi pamoja katika moto,

> alisogea akapenyeza mkono kile kitezo kinachotowa biwi la moshi linalonuka na kunukia pamoja, akimzungushia mwanawe kichwani na huku akiomboleza kwa maneno yenye lafudhi au matamko kama Kiswahili cha Pemba cha ndani au Kiswahili cha asili cha Makunduchi; lakini la mimi wala wewe hatukufahamu.
>
> Bi Kazija mama yake Kipwerere, anafahamu maneno ya shetani wa mwanawe, na kaagua kuwa kuna jambo baya mbele yao linakuja- kama la kifo- na kafara lake linataka mbuzi mwekundu achinjwe 'waruke damu' (uk. 11-13).

Katika maisha ya kawaida katika jamii wahusika kama hawa mtafiti anakutana nao. Kama mtafiti alivyoeleza hapo kabla kwamba matendo kama haya yanaonekana yakitendwa na baadhi ya waganga wa jadi ambapo kiukweli hayawezi kuthibitika kwa misingi ya kisayansi. Mbali na hayo ni mjuzi wa lugha ya mashetani ambayo ni vigumu kuelewa watu wengine. Hii ni kutokana na manuwizi yake pia kuweza kufumbua fumbo la shetani wa mwanawe na kutaja kafara lake.

Vile vile, dhamira ya imani za jadi imesawiriwa kupitia mhusika maiti. Msanii ameeleza kuwa watu waliokuwa wakiishi karibu na Mzimu wa watu wa kale walikuwa wakijiwa na maiti usingizini. Msanii anasawiri dhamira hii wakati anaposema:

> Mara nyingi wenyeji wa pale watakwambia wamejiwa na maiti hao usingizini hawana miili tena ila wamebakia vivuli tu; na wao huwataabisha sana walalapo. Mpaka uje wakati na wao waone ni mno tena, watu wote wa kiamboni-ila Bwana Ali hajapata kutoa kitu-wanunue ngombe na mapaji mengine watowe kafara la kuwatuliza mizimu ilale ili na wao wapate kutulia (uk.17).

Dondoo hili linaonesha namna msanii alivyoichora jamii ikiwa na imani za kijadi. Baadhi ya watu wamekuwa wakiogopa baadhi ya mazingira kwa kuhofia kupata madhara. Ama baadhi ya watu huogopa kutokana na ndoto ambazo zimekuwa zikiwatokea usingizini wakati wa usiku wakiwa wamelala.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti ameona namna dhamira ya imani za jadi inavyowiana na nadharia. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba imani za kijadi zimeenea katika jamii za Tanzania na Afrika kwa jumla. Kutokana na ukweli huo, soko la waganga wa kienyeji limeongezeka kwa kiasim kikubwa.Jambo hilihuwaweka watu wengine katika matatizo. Kwa mfano hujuma dhidi ya walemavu wa ngozi (albino) pamoja na mauaji na upoteaji wa watu ambao hutumiwa katika imani za kichawi. Imani hii inaungwa mkono na baadhi ya watu wa matabaka mbalimbali kama vile watu wa tabaka la chini na hata baadhi ya viongozi.

4.5.2 Uongozi Mbaya

Dhamira ya uongozi mbaya imejitokeza kupitia wahusika tumbili ambao wamesawiriwa kiuhalisiajabu. Tumbili na makima hao walikuwa wakiharibu mazao ya watu lakini watu hawakuweza kuchukua hatua yoyote kwa imani kwamba huenda ikawa ni vizuu wa watu saba wa kale. Kwa mantiki hiyo walikuwa na hofu ya kutowakera. Kuhusu hili msanii anasimulia kwa kusema:

> Jinsi mzimu wa watu wa kale unavyotisha namna hii hata wale tumbili na makima walivyozaliana wakajazana ndani ya kichaka hicho, pindi wakigundulika wanaharibu konde za watu mashambani mwao, wenyeji wale hukataza wasipigwe, maana walisema kwamba huenda ikawa wanyama wale ni vizuu vya wale watu saba wa kale (uk. 17).

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amegundua kuwa makima na tumbili wanaoelezwa katika dondoo hili ni wahusika wa kiishara ambao wanawakilisha tabaka la juu lililoshika hatamu za uongozi. Tabaka hilo limekuwa likiwatendea maovu watu wa tabaka la chini lakini watu hao wanaonyonywa na kukandamzwa hawana uthubutu wa kupinga uovu huo. Hili linatokana na ukweli

kwamba tabaka la juu limejenga vitisho dhidi ya tabaka la chini. Kwa mantiki hiyo, tabaka la juu limebakia kama miungu watu ambao hawawezi kukosolewa na tabaka la chini. Jamii nyingi za Afrika zimeathiriwa na uonevu unaofanywa na baadhi ya watoto na jamaa za viongozi wa juu wa serikali au taifa. Watu hao wamekuwa wakifanya ubadhirifu wa mali ya umma, huhodhi mali za watu na hata kukiuka haki za binadamu.

4.5.3 Ukoloni

Dhamira ya ukoloni inajitokeza kupitia mandhari ya kichaka cha mzimu wa watu wa kale. Msanii anaeleza kuwa watu walikuwa na hofu ya kupita katika msitu huo kwa hofu ya kudhurika. Watu walilazimika kupiga hodi wakati wanapotaka kupita sehemu hiyo. Msanii alisimulia hivi:

> "Mzimu wa Watu wa Kale ni kichaka kinachosumbua watu wa sasa. Wale wanaojua vitisho vya mizimu, hawaipiti ovyo ovyo njia hiyo bali huchagua nyakati za kupita. Watakwambia kuwa Adhuhuri na Magharibi usipite mahali hapo, maana wakati huo mizimu wanasali. Na pindi ukipita wakati mwengine, basi lazima juu yako kupiga hodi, na ukisahau kupiga hodi, basi litakalokupata usilie na mtu- labda ulie na mizimu tu (uk. 16)."

Dondoo hii inaonyesha namna tawala za kikoloni zilivyojenga hofu miongoni mwa wanajamii. Wakoloni waliweka masharti ya kufuatwa na watawaliwa ambayo yalipaswa yasikiukwe. Wanajamii nao walijenga hofu ya kukiuka masharti ya wakoloni ambao ni watawala wao. Kwa sababu hiyo Waafrika walijikutia wakitii maamrisho ya wakoloni bila ya kujali haki na utu wao. Hata hivyo ikumbukwe kwamba Waafrika walikuwa hawakubaliani na mateso hayo toka kwa Wakoloni ndio maana kufikia miaka 1950 walianzisha harakati za kudai uhuru ili kuondokana na mateso ya wakoloni.

Katika kusawiri dhamira hii ya ukoloni msanii pia anaeleza namna ndani ya mzimu wa watu wa kale kulivyokuwa na mambo ya kuogopesha. Mathalani, msanii anaeleza kuwa Bwana Msa alipochungulia ndani alibaini kwamba kulikuwa na kiza kama uwanda wa Akhera. Pia, ilisikika sauti moja kubwa kama maporomoko ya maji. Msanii anasimulia kwa kusema:

> "Bwana Msa alichungulia tena. Ndani mulikuwa na kiza kama uwanda wa Akhera, kiza kilikuwa kimetapakaa, kinavuja! Sauti za komba na mabundi- wasiojua, kwa sababu ya kiza kilichozagaa, kama kimekwisha kucha- zilihanikiza sauti zote za vidudu zinazosikilikana kichakani au mashamba wakati wa usiku. Lakini juu ya sauti zote hizo, ilipaa sauti moja tu kubwa kuliko zote iliyokuwa ikiendelea bila ya kusita na ikivuma kama maporomoko ya maji. Bwana Msa alishindwa kuelekeza sauti ile ni ya nani, na ndiyo iliyomrudisha uso wake nyuma alipojaribu kuchungulia ndani. Kwa kiasi tu, alielekeza kuwa ni sauti ama ya gurudumu, kama gurudumu la motokaa, linazunguka na kwenda mbio humo ndani ya mzimu, au mkokoto wa kitu kirefu kizito kama chatu, kinajikokota kwa upesi juu ya majani makavu. Lakini mara ilimjia hisi kwamba kila dakika sauti ile ilizidi kuwa kubwa kwa sababu ilikuwa ikisogea mbio mbio kukaribia, 'mlangoni,'pale walipo wao. Nani anaendesha gari ndani ya mzimu? Tuseme wale maiti?
>
> …Bwana Msa alikitoa kichwa chake, akampisha mwenziwe, na huku akimwambia "Hebu sikiliza, Najum. Mna sauti ndani kama mna watu wanaendesha gari, tena linakuja kuku huku tuliko; je unalisikia?"
>
> Najum akatia kichwa chake kusikiliza, na huku akisema, "Labda mizi-'' (uk. 22- 23).

Dondoo hili linaonesha namna wakoloni walivyokuwa wamejenga ngome imara ya kuhakikisha kwamba katika utawala wao hakupenyi lolote ambalo lingeweza kuleta athari. Sauti za kutisha zinazoelezwa katika dondoo hili ni maneno makali ya baadhi ya viongozi yanayohusu maonyo ya kutothubutu kukaribia utawala wa kikoloni. Kutokana na hali hii Waafrika walilazimika kutii tawala za kikoloni.

Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba maelezo haya yanalandana na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Kama wasemavyo Njogu na Wafula (2007)kwamba moja ya msingi wa nadharia hii ni kuyaangazia yale yanayojadiliwa na msanii na namna yanavyotokea au yalivyowahi kutokea katika jamii. Hivyo basi, ni wazi kwamba wakoloni waliwajenga hofu na woga Waafrika ili kuendelea kuwatawala katika nchi zao. Kwa Mfano mwandishi Shaaban Robert alilazimika kutumia nadharia ya Uhalisiajabu katika kazi zake za fasihi kwa sababu ya kukwepa mkondo wa sheria.

4.5.4 Utabaka

Mandhari ya makaburini yaliomo ndani ya mzimu wa watu wa kale ni mandhari inayotuibulia dhamira ya utabaka. Msanii alisimulia katika riwaya hii kwamba mara baada ya Bwana Msa kuyapita makaburi mchanga ulikuwa kidogo na kutokea jangwa. Pia, kulikuwa na kijito cha maji lakini kijito hicho hakikuwa na maji isipokuwa unyevunyevu. Msanii anatusimulia hivi:

> Kuyapa makaburi kisogo tu, mara mchanga ulisita kuwa mwingi, na jangwa likageuka uwanda. Kwa mbele kidogo, kilipita kijito cha maji- si kijito kitu, la vimajimaji na unyevu unyevu tu katika ardhi (uk. 37).

Katika dondoo hili limesawiri namna jamii za Uswahilini wakati wa utawala wa ukoloni zilivyojengwa kitabaka. Wanajamii waligawanyika na hata maisha ya watu yalijengwa kitabaka. Wapo walioishi maisha ya walala hoi (tabaka la chini) na maisha ya walala heri (wakoloni). Hata miji ilijengwa kutegemea matabaka.

Dhamira ya utabaka pia inajadiliwa kupitia Bi Kazija, mama yake Kipwerere. Kama msanii alivyoeleza kwamba Bi Kazija alikuwa na uwezo wa kufahamu maneno ya

shetani. Kutokana na uwezo huo aliweza kubaini kwamba kulikuwa na jambo baya linakuja. Msanii alisimulia tukio hili hivi:

> Kwa wakati ule Ahmed alirudi kwa wenziwe akawaeleza kuwa Bi Kazija, mama yake Kipwerere, anafahamu maneno ya shetani wa mwanawe, na kaagua kuwa kuna jambo baya mbele yao linakuja jambo kama la kifo-na kafara lake linataka mbuzi mwekundu achinjwe 'waruke damu'. Lakini alipotoka pepo kichwani, Kipwerere kashikilia lazima aende mtu Baraste kumsikiliza mumewe, na kama hapana mtu wa kwenda, basi atatoka yeye mwenyewe aende, maana wakati ule ulikuwa unapata saa mbili naye hajarudi bado (uk. 13).

Katika dondoo hili mtafiti anaona namna jamii ilivyokuwa imejengeka kimatabaka. Wapo Waafrika ambao waliweza kubaini matendo ya wakoloni (maneno ya shetani), kwa sababu hiyo waliweza kujiepusha na baadhi ya hujuma za kikoloni. Kutokana na sifa hiyo ndio maana Bi. Kazija aliweza kutambua kile ambacho kitampata Bwana Ali.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa suala la utabaka linalojadiliwa na msanii katika riwaya hii linalingana na nadharia hii. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba wakoloni walijenga utabaka ili kufanikisha matakwa yao ya kuwatawala Waafrika. Ali (2015)anaeleza kwamba watawala wa kikoloni walifuata mawazo ya "wagawe ili uwatawale." Kutokana na ukweli huu ndio maana hata jamii ya Wazanzibar wanaoishi katika kisiwa cha Unguja hadi leo kwa asilimia kubwa wenye asili ya Asia wanaishi maeneo ya Mji Mkongwe na watu wenye asili ya Afrika wanaishi maeneo mengine ya Kisiwa hicho. Hii ni taswira halisi ya utabaka uliotengenezwa na wakoloni.

4.5.5 Mauaji

Katika makaburi ya mzimu wa watu wa kale mtafiti ameibuwa dhamira ya mauaji. Katika kuijadili dhamira ya mauaji msanii ameelezea kuwa Bwana Msa waliikuta maiti ya Bwana Ali imeroa damu. Pia, maiti ya Bwana Ali ilikuwa imepakata boga lakini haikua na kichwa. Tukio hili lilidhaniwa na Bwana Msa kwamba ulikuwa ni mchezo mmoja wa vile vizuu vinavyopatikana katika mzimu wa watu wa kale. Inasimuliwa na msani anaposema hivi:

> “Ndiye kweli Bwana Ali, lakini hana kichwa. Koti lake la kaki lilikuwa limeroa damu. Miguu yake kainyoosha mbele yake na juu ya mapaja yake alikuwa amepakata boga tu wala si kichwa chake, kama ilivyoonekana kwa mbali. Nadhani ulikuwa mchezo mmoja wapo wa vile vizuu vya watu wa kale, au makima wa kule kichakani kumpakatisha boga maiti yule. Kwa kweli, yalikuwa mandhari mabaya sana, ya kusisimuisha mwili” (uk. 36).

Katika dondoo hili msanii anaonesha namna suala la mauaji lilivyokuwa ni suala la kihistoria katika bara hili la Afrika. Mauaji yalianza kufanyika wakati wa ukoloni. Hii ni kusema kuwa wakoloni walifanya mauaji ya watu bila ya kujali utu na haki ya mtu. Mauaji yaliyofanywa dhidi ya Bw. Ali ni matendo ya kinyama na ya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Katika sehemu nyengine ya riwaya hii ya *Mzimu wa Watu wa Kale* msanii ameeleza kuhusu tukio la mauaji ambalo ni suala linaloibua mshituko miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, Najim alipatwa na mshituko baada ya kuiona maiti ya Bwana Ali imepakata kichwa chake. Aidha, mauaji yanapotokea kuna wale wasioelewa kinachoendelea hudhani kuwa huenda ni sahihi kufanya hivyo. Baadhi ya watu huyahusisha mauaji hayo na imani za kishirikina. Kuhusu tukio hili msanii anasema:

> Najum akazidiwa na hofu. Kumbe yule aliyekuwa amekaa pale chini ya kaburi hali amenyoosha miguu yake na kupakata kichwa chake, alikuwa Bwana Ali! “Nini kilichompeleka mzimuni magharibi, wakati watu wanakatazwa kupita, na kukaa chini ya mzimu kama kwamba yuko kwake! Ikiwa habari zisemwazo za mizimu ni kweli, (na kwa namna hii zinaonyesha kuwa ni kweli) basi yaliyompata Bwana Ali ni stahili yake, maana alijuwa kuwa wakati wa magharibi hakuna ruhusa ya kupita, naye alikwenda kusudi kughasi. Lakini alitaraji nini?” (uk. 35-36).

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kwamba suala la mauaji yaliyofanywa na wakoloni yaliwafanya Waafrika wachoke na udhalimu huo. Ndio maana kufikia mwishoni mwa miaka ya 1950 nchi za Afrika zilianzisha wimbi la kudai uhuru toka kwa wakoloni. Wimbi hili lilichangiwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliokuwa ukifanywa na wakoloni dhidi ya Waafrika. Kwa mfano kuwatesa, huwafunga gerezani na hata kuwaua wale walioupinga utawala wao.

4.5.6 Umuhimu wa Kutunza Kumbukumbu

Data zilizokusanywa kutoka katika riwaya teule zimebainisha kwamba mbinu ya uzungumzinafsi imetumiwa na msanii kama sehemu ya mtindo wa uhalisiajabu ili kuibua dhamira ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu. Mbinu hii imetumiwa na mhusika Bwana Msa wakati anapojiuliza kuhusu karatasi aliyoiokota ambayo ilikuwa ni stakabadhi ya kuuziana shamba. Ajabu ni kwamba karatasi hiyo haikuwa na tarehe wala saini. Msanii anasema hivi:

> Bwana Msa aliuliza, “Mtu akikaa akichorachora upuuzi tu, atachora kitu cha maana au cha upuuzi tu vile vile?” Lakini sauti alivyokuwa akisema bila ya kumtupia jicho sahibu yake, alionyesha kuwa anasema na nafsi yake tu kwa sauti (uk.30).

Katika dondoo hili msanii anaonesha umuhimu wa kuandikiana kumbukumbu kama sehemu ya ushahidi wakati watu wanapouziana vitu mbalimbali. Pia, msanii

anaonesha kwamba ili kuhakikikisha kuwa muamala uliofanyika ni sahihi ni vyema kuhakikisha nakala ya mauziano ioneshe masuala muhimu kama vile saini ya muuzaji na tarehe ya siku ya manunuzi.Kukosekana kwa taarifa hizi muhimu hupelekea karatasi hiyo ikaonekana kama jambo la upuuzi na isiyofaa. Vile vile, baada ya stakabadhi kukamilika inampasa yule aliyenunua awe nayo yeye mwenyewe binafsi. Katika kushadadia suala hili msanii anasimulia hivi:

> Najum alitazama akaona sasa Bwana Msa anasema maneno ya upuuzi; maana mambo mawili haya aliyoyataja yanapingana yenyewe kwa yenyewe na yanarejea kule kule kuwa karatasi ile ni upuuzi. Ikiwa ile ni stakabadhi hakika, basi yule Banyani alikuwa mpumbavu asiipokee kwa Bwana Ali akawa nayo mwenyewe. Na vile vile ilivyokuwa stakabadhi yenyewe haina sahihi wala tarehe, basi inafuta yale masala hakika yake, na kuifanya stakabadhi ile vile vile ni upuuzi tu. Kinyume cha mambo, leo, inaonyesha dhahiri kuwa Bwana Msa ana wazimu! (uk. 30-31).

Kutokana na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa mwandishi anawakosoa watu wenye tabia ya kuandika stakabadhi bila ya kuwa na saini wala tarehe. Hapa wanajamii wanafundishwa namna ya kufanya mauzo na kununua vitu. Kama inavyotambulika kwamba ulimwengu leo ambaoumejaa kila aina ya matatizo na migogoro yanayosababishwa na umiliki wa mali. Kesi zilizokithiri katika mahakama ni za dhuluma kuhusu ardhi kwa vile watu wengi wamekuwa wakiuza vipande vya ardhi kwa mtu zaidi ya mmoja.Kwa sababu hii jamii inatakiwa kuweka kumbukumbu za skabadhi za manunuzi ili kuepuka migongano isiyokuwa ya lazima.

4.5.7 Upelelezi

Aidha, kipengele chengine cha uzungumzi nafsi unajitokeza pale Spekta Seif alipokuwa akisema na kujiuliza nafsi yake kuhusu kifo cha Bwana Ali ambapo

alishangazwa kwa kuona kichwa mbali na kiwiliwili mbali. Tukio hili linasimuliwa na msanii hivi:

> Njiani, walikuwa wakienda kimya ila yeye peke yake alikuwa akipita akisema polepole kama anasema peke yake. “Nani hasa aliyemwua Bwana Ali? Ilikuwaje hata kichwa kikawa mbali na kiwiliwili mbali? .....” (uk.51).

Katika dondoo hili msanii anaonesha umuhimu wa suala la upelelezi kuwashirikisha wanajamii ili kupambana na maovu yanayotendeka. Msanii anaonesha kuwa jeshi la pilisi sio chombo pekee ambacho kinaweza kufanya upelelezi na hatimae kuibua maovu yanayotokea katika jamii. Kutokana na ukweli huo ndio maana Tanzania imeanzisha dhana ya ulinzi shirikishi (Polisi Jamii) ili wanajamii kushiriki katika ujenzi wa jamii ikiwa ni pamoja na suala zima la kupambana na uhalifu. Ushiriki wa Bwana Msa katika riwaya hii unaonekana ni wa kiwango cha hali ya juu ukilinganisha na hata ule wa Najim katika kuyapeleleza matukio yanayotendeka kama yale ya uhalifu.

Katika sehemu nyengine Spekta Seif anatumia mbinu ya uzungumzi nafsi kama sehemu ya uhalisiajabu inayojadili dhamira ya upelelezi. Taarifa hizi zimepatikana kupitia Spekta Seif anapojiuliza maswali mbalimbali wakati akifikiri kuhusu mauaji ya Bwana Ali. Mtunzi anasimulia tukio hili hivi:

> Akasimama kuitazama maiti mara ya mwisho, “Tazama shingo ilivyo safi. Lazima aliyeua alikuwa na nguvu nyingi, maana hapana ila dharuba moja tu aliyompiga, akakirusha kichwa; mambo gani haya? Inaonyesha kuwa ni mtu mmoja tu aliyeua. Aidha, yaonyesha kuwa hakuwa peke yake katika kazi hii. Wenziwe gani hao? Na kwa nini akaweka boga mapajani mwake? Lo, mambo haya yataharibu akili za watu wote waliopo hapa Baraste, na itikadi ya Mzimu wa Watu wa Kale itazidi kuwa na nguvu” (uk. 54).

Katika dondoo hili Najim anapata dalili ya namna mauaji ya Bwana Ali yalivyotendeka. Hata hivyo pamoja na uelewa huo mtafiti anabaini kuwa Najim alishindwa kugundua ni nani hasa aliyetekeleza mauaji hayo. Katika matukio kama haya inapasa jeshi la polisi kushirikisha baadhi ya watu ambao wanauelewa wa kazi hizo kama tulivyokwishaeleza hapo juu. Ndio maana baada ya Bwana Msa kushirikiana na Najim wanabaini ni nani aliyetekeleza mauaji hayo.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunabaini kwamba dhamira ya upelelezi inayojadiliwa na Mohamed Said Abdulla inaenda sambamba na hali ilivyo katika jamii ya leo. Upelelezi unafanywa na jeshi la polisi katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha jamii inabakia katika hali ya amani na usalama. Pia, kutokana na umuhimu wa jambo hilo jeshi la polisi limekuwa likiwashirikisha wanajamii wa ngazi mbalimbali kwa mfano vikundi vya polisi jamii na sungusugu vinasaidia katika jamii zetu.

4.5.8 Uganga

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* data zinaonesha kuwa suala la uganga wa jadi limejadiliwa. Dhamira hii inajitokeza kupitia ugonjwa wa Kipwerere. Msanii ameeleza kuwa waganga walikuwa wakiagua kwamba Kipwerere alirogwa na wachumba waliokuwa wakimchumbia ama alikumbwa na shetani wakati akipita katika msitu huku akiwa anakula ndizi. Mwandishi anasimulia tukio hili hivi:

> Mambo yalipokithiri, wazee wake walifika kwa waganga kutazamia, nao kila mmoja alisema lake. Wengine walisema kuwa amerogwa na wachumba waliokuwa wakimtaka wakamkosa. Wengine walisema kuwa amedhuriwa katika kile kichaka kiitwacho ‘Mzimu wa Watu wa Kale’, alipokuwa akipita siku hizo bado kigori na huku anakula ndizi ya kipukusa; kwa hiyo, shetani wa mzimuni alimshika na kumpanda kichwani wala hatamtuliza na kumpa nafasi ila apate chano cha

> ng’ombe. Wazee wa Kipwerere walipendekezewa na aguo la pili kuwa mtoto wao kasibika na shetani, maana waliona inamkinika kuliko lile aguo la kwanza lililoagua marogo ya mchumba waliomkosa, kwani hakutokea hata mmoja katika hao waliootea uchumba, kwenda kumposa- kabla ya Bwana Ali - akakataliwa.
>
> Na kwa hiyo kila dhofu ilihali ikizidi kumkondesha Kipwerere wazee wake humshika mumewe Bwana Ali atowe ng’ombe mmoja ili apewe chano mtoto wao apate kupumzika; lakini Bwana Ali huzidi kuwapa ahadi za mbele tu, mwaka baada ya mwaka, mpaka leo hii (uk. 8-9).

Katika dondoo hili msanii anaonesha namna suala la uganga wa kienyeji linavyochukuliwa kama sehemu ya tiba miongoni mwa wanajamii. Hata hivyo matibabu haya ambayo hayawezi kuthibitika kwa misingi ya kisayansi bado yana mapungufu. Mathalani msanii anaonesha kuwa kulikuwa na mitazamo miwili kuhusu chanzo cha ugonjwa wa Kipwerere. Utata kama huu hautupi uhalisia wa chanzo cha ugonjwa huo. Pia, hali kama hii huweza kusababisha mifarakano miongoni mwa wanajamii pamoja na matumizi ya pesa ambayo hayatafanikisha tiba ya ugonjwa husika.

Kutokana na nadharia ya Mwitiko wa msomaji mtafiti anabaini kuwa dhamira ya uganga kama inavyojadiliwa na msanii inawiana na hali ilivyo katika jamii nyingi za Afrika Tanzania ikiwemo. Hapa Tanzania uganga wa jadi umekuwa ukichukuliwa kama sehemu ya tiba muhimu sana kwa jamii. Mathalani, baadhi ya watu huamini kuwa mashetani wamekuwa wakiwaathiri watu. Kutokana na hali hiyo wapo waganga wa kienyeji ambao huamini kwamba wanaweza kupambana na shetani wakati anapomdhuru mtu.

Ingawa hadi sasa suala la uganga wa kienyeji limewagawa wanajamii kuhusu kukubalika. Mathalani wapo ambao huamini kwamba waganga hao wengi wao ni

watu ambao wameandaa mipango maaluumu ili kujipatia pesa kwa urahisi kutokana na kuwadanganya watu. Tapo hili linaona kuwa waganga wa kienyeji hawana nafasi bali ni matapeli. Mathalani, katika kulieleza suala la uganga wa kienyeji Mbia (1960), katika tamthiliya Three Suitors: One Husband anamchora mhusika Sanga-Titi ambaye anawadanganya wanakijiji ili kujipatia pesa. Kutokana na tabia ya uongo wa baadhi ya waganga wa kienyeji ndio maana hata serikali ya Tanzania imekuwa ikipambana vikali na baadhi ya waganga wa kienyeji. Ama tapo la pili ni lile linaloamini kwamba waganga wa kienyeji ni mbadala wa waganga tulionao hospitalini. Kwa mtazamo huu kundi hili linaona kuwa waganga wa kienyeji wana umuhimu na wamekua wakiisaidia jamii katika masuala ya tiba.

4.5.9 Unyonyaji na Ukandamizaji

Katika riwaya hii kuna mjadala kati ya Najim na Bwana Msa kuhusu hali ya mtu anapokuwa amechagawa. Kupitia mjadala huu msanii anaibuwa dhamira ya unyonyaji na ukandamizaji. Msanii amemsawiri shetani kama ishara ya tabaka la juu ambalo linamkandamiza binaadamu ambaye ni ishara ya tabaka la chini. Kuhusu tukio hili msanii anasimulia kwa kusema:

> Kwamba wewe unadhani- kama wanavyodhani watu wengine- kwamba mtu akichagawa hujiwa na shetani au hupandwa na pepo aliyetoka bahari ya saba au ardhi ya saba, yaani yule binadamu kwa wakati ule huwa kama ‘kiti’ chake. Vyema, lakini ‘kiti cha shetani ni bianadamu, na binadamu ana sehemu mbili, kiwiliwili na roho, sasa, mtu akichagawa, shetani hukaa wapi hasa, mwilini au rohoni mwake? (uk.12).

Kupitia dondoo hili mtafiti amebaini jinsi watu wa tabaka la kikoloni walivyokuwa wakiendeleza unyonyaji na ukandamizaji miongoni mwa watu wa tabaka la chini. Ukandamizaji huu unalingana na ule unaojadiliwa na Hussein (1971) katika

tamthiliya ya *Mashetani* na Mohamed (2016), katika tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ambapo wanaona kuwa mashetani ni wakoloni ambao wamekuwa wakinyonya na kukandamiza nchi za dunia ya tatu.

Kwa kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kwamba masimulizi haya yanafanana na hali ilivyokuwa katika bara la Afrika wakati wa ukoloni. Huu ni muendelezo wa masimulizi yanayoihusu jamii. Kama asemavyo Mulokozi (2012), kwamba katika fasihi ya Kiswahili masimulizi ya kihistoria yamekuwepo tangu kale. Vitabu vya tarehe husimulia matukio ambayo yanatokana na masimulizi ya mdomo. Hivyo ni wazi kwamba katika sehemu hii msanii anaibua ukandamizaji na unyonyaji uliofanywa na wakoloni kwa mbinu ya kisanaa.

4.5.10 Mfumo wa Kiuchumi

Tukio jengine la uhalisiajabu linajitokeza wakati msanii aliposimuliwa mapisi ya watu wa mapangoni. Tukio hili linaibua dhamira ya mfumo wa kiuchumi. Mifumo mikuu ya uchumi duniani ni miwili. Mfumo wa kibepari na mfumo wa ujamaa. Hivyo katika kulijadili suala la mfumo wa kiuchumi ulimwenguni msanii anasimulia hivi:

> Watu wa mapangoni walichukua kombe ya chaza anayeitwa Panga, wakaijaza maji yao ya siri yanayojulikana kwa waganga tu kuwa ni ‘Maji ya Mkondo wa Mauya;’ wakasema wakiomboleza maneno yasiyofahamika; kisha wakayamwaga maji yale katika jiwe la marjani, na hapo hapo ukatoka moshi mwingi. Moshi ule ulipokwisha, watu wa mapangoni walikuwa tayari kuagua. Walisema kuwa watu wale saba wametoka katika bara la Waajemi, katika mji wa Al Hasa; wametoka watokako wakipita kuitafutaAkhera iliko; na walipofika Jongomeo, Mwenyazi Mungu akawateremshia mauti; roho zao zikahama miilini mwao. Lakini kweli hasa kwa mwenye kutambua (uk. 16-17).

Kupitia dondoo hii msanii anaonesha namna mfumo wa ujamaa ulivyopoteza nguvu zake na hatimaye nafasi hiyo kuchukuliwa na mfumo wa kibepari. Mfumo huu wa ubepari nao ukawa na athari hasi kwa bara la Afrika. Kama asemavyo Mulokozi (2012) kwamba mfumo huu unaambatana na ufisadi, rushwa, ukwepaji kodi, magendo, uuzaji wa madawa ya kulevya, usaliti, usaliti na upotoshaji wa habari. Matendo haya yameufanya mfumo wa ubepari kuigeuza dunia kama shamba la wanyama, mwenye nguvu kumla mdogo.

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti anabaini kwamba suala la mjadala unaohusu mfumo wa uchumi limezua mtafaruku mkubwa miongoni mwa wanajamii. Wapo Watanzania wanaoamini kwamba mfumo wa ujamaa hapa ulikuwa na mwelekeo mzuri lakini ulikumbwa na changamoto. Mathalani, Omary (2011)anaona kuwa mfumo wa ujamaa hapa Tanzania ulikuwa ni mfumo uliofana lakini viongozi wasaliti ndio walioufanya kuonekana kuwa haufai. Viongozi hao walisaliti malengo ya ujamaa chini kwa kuvuruga matakwa ya Azimio la Arusha.

4.4.11 Nafasi ya Mwanamke

Nafasi ya mwanamke imejadiliwa na msanii wakati anaposimulia namna Bi Kazija alivyogundua kuwa kulikuwa na hatari imemkabili Bwana Ali. Msanii ameeleza tukio hili pale aliposema:

> “Yule bibi hapana shaka, alikuwa, na wasiwasi tangu hapo. Wakati mwingi huambiwa, ‘roho ni bao’ yaani huona yatakayo kuja kabla hayajatokea. Maneno haya, mara nyingi huwa ni kweli, roho yake yule bibi iliruka kwenda kutazama matokeo ya siku ile, na ilivyokuwa mumewe mpaka sasa hivi hayuko nyumbani kama desturi yake, roho yake yule bibi ilianza kuagua mambo iliyoyaona katika ukaguzi wake. Roho ilistuka ilipoona ‘kiza,’ ‘hapana’ yaani ‘kiza kitupu’; na, kwa kweli, kiza kitupu hapana ila mauti. Roho ilizidi kutegua ilipoona kitu ‘safi kabisa,’ tena ‘chekundu.’ Kitu gani hicho kilichokuwa safi

> kabisa tena chekundu isipokuwa damu? Yaani, kwa ufupi, yule shetani, au roho ya yule bibi, ameagua kuwa Bwana Ali ameuwawa-" (uk. 12).

Katika dondoo hili msanii ameelezea namna baadhi ya wanawake katika jamii walivyo na mapenzi ya kweli kwa waume zao. Mfano wa wanawake hao ni Bi. Kipwerere ambaye kutokana na kuwa na mapenzi ya kweli anaingiwa na wasiwasi kutokana na Bwana Ali kucherewa kurudi nyumbani. Mapenzi ya kweli yanaakisi wanawake wengi wa Uswahilini ambao huwahurumia na kuwatunza waume zao. Mulokozi (1999)wakati akifanya uchambuzi wa Utenzi wa Mwanakupona anaonesha kwamba wanawake wamekuwa wakiwatumikia wanaume kwa kila jambo. Mulokozi anaiona hali hii kuwa ni sawa na kuwadhalilisha wanawake. Hata hivyo ukweli ni kwamba katika maisha ya Uswahilini mwanamke hulazimika kumtii muume wake ili kuonesha upendo na kuleta kitulizano katika maisha ya ndoa.

Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba jamii za Afrika, Tanzania ikiwemo suala la nafasi ya mwanamke kama kiumbe mwenye mapenzi ya kweli katika ndoa linalandana na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Wanawake wamekuwa wakiuchukuliwa kama sehemu ya kitulizano cha wanaume na wanahakikisha wanatendea mema waume zao. Iwapo itatokea mwanamke hana mapenzi ya kweli hasa wale walio katika ndoa hujikuta wakitalikiwa.

4.5.12 Utamaduni

Mbinu ya umahuluti wa kiutamaduni, kitanzu na mwingilianomatini kama sehemu ya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imetumika ili kuibua dhamira ya utamaduni. Ali (2015)anasema kwamba utamaduni ni jumla ya maisha ya

wanajamii. Kila jamii ina utamaduni wake ambao huweza kuutambulisha na unahitaji kutiiwa na kila mwanajamii hio bila ya kujali tabaka alilo. Katika kutii utamaduni wa jamii Muhammed Said Abdulla anaeleza:

> "… Bwana Msa alitangulia, akapiga magoti akasema "Hodi" mara tatu, kisha akatia uso wake ndani kuchungulia. Kuona vile Najim alistaajabu si haba. Bwana Msa aliyekuwa akisubu mambo ya mizimu kwa maneno ya bezo namna ile imemjia kuutukuza mzimu namna hii? Najim hakuweza kusubiri, bali aliuliza kama anachokoza, "Unapiga 'hodi' kwani wewe unaamini nini kitendawili chao cha mizimu?" (uk. 27).

Dondoo hili linaonesha namna Bwana Msa anavyopiga hodi katika msitu huo kama ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Sasa hakuwa na hiari ila kuhakikisha anatii miiko ya jamii iliopo. Ingawa katika dondoo hili linafafanua msimamo wa Najim kuhusu suala la utamaduni wa jadi la kuamini mizimu. Ni kuwa bado haamini na hakubaliani na utamaduni huo.

Suala la utamaduni pia linaendelezwa na msanii kupitia mbinu ya muingiliano wa kiutamaduni na kitanzu kupitia wahusika Bwana Msa na Najim. Bwana Msa anamueleza Najum kwamba iwapo amemstua itakuwa amemroga. Mtafiti alieleza hapo kabla kwamba hii ni imani ya kitamaduni ambayo katika jamii ya Uswahilini huchukuliwa kama utamaduni wa Mswahili. Msanii alisimulia tukio hili hivi:

> "Ahlan, Najum! Nimekustua au nimekuzindua? Ikiwa nimekustua, itakuwa nimekuroga; lakini, ikiwa nimekuzindua itakuwa nimekuzingua. Bali ilivyokuwa hapo ulipochutama pana zindiko langu, na litayari kumzingia mtu yoyote atakayejitia umbea, hapana shaka kwamba kutokea kwangu hivi sasa nikasimama mbele yako namna hii, kumekuzingua" (uk.4).

Dhamira ya utamaduni pia inajitokeza kama sehemu ya umahuluti wa utamdauni kwa mhusika Mama Kipwerere. Mama huyu baada ya kugundua kwamba mtoto

wake anaumwa alibaini kwamba tatizo ni shetani. Huu ni utamaduni ambao unaonekana kufuatwa na kuaminiwa na wanajamii wengi wa Afrika. Msanii alisema:

> Mama Kipwerere alipoona hali ya mwanawe namna ile, alifahamu kwa upesi kuwa ugonjwa ule wote unatokana na yule shetani anayekwambwa naye na kwa hiyo alijaribu kumpumbaza mwanawe na kumletea shauri la 'kumshika sikio' shetani huenda akampa nafasi kidogo. Kipwerere, alivyokuwa na yeye yumo katika itikadi zile, na vile vile hawezi kuvunja shauri la mzee wake, aliridhi kufanyiwa yale, ndipo bikizee akachukua kitezo, akaenda uani na jikoni kutafuta moto (uk. 9).

Katika dondoo hili msanii anaonesha jinsi masuala ya utamaduni yanavyotendeka. Katika jamii za Kiislamu wanaamini kwamba shetani huwa analeta madhara katika jamii. Mutiso (2012)alipokuwa akifanya uchambuzi wa *Utenzi wa Rasil`ghuli* anasema kwamba "ghul" ni shetani au pepo mbaya alaye watu. Shetani huyu anaweza kumfanyia mtu sihiri au mazingaombwe na yumkini ni mchawi wa kiume ambaye anaweza kujigeuza kwa maumbo tofauti tofauti. Kwa kawaida majini ya aina hii huweza kuwa katika maumbo mbalimbali ya wanyama na wanadamu.

Kwa kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni dhahiri kwamba dhamira ya utamaduni kama inavyojadiliwa katika riwaya teule inawiana na nadharia hii. Utamaduni wa kuamini shetani umeenea sana katika jamii za Uswahilini. Katika jamii hizi watu huamini kuwa shetani huweza kumdhuru mtu na hata wapo baadhi ya watu wanaoaminika kwamba wanafuga mashetani na kuwatumia katika miktadha mbalimbali ya maisha yao.

4.6 Hitimisho

Sura hii imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Sura hii imeanza kwa kueleza usuli wa mwandishi Mohamed Said Abdulla na muhtasari wa riwaya ya *Mzimu waWatu wa Kale*. Vile vile, sura imefanya uwasilishaji wa data za utafiti zinazohusu vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale,* baadae sehemu hii imewasilisha data zinazohusu vipengele vya Uhalisiajabu na namna vinavyoibua dhamira katika riwaya ya Uhalisiajabu. Mwisho sura hii imemalizia kwa kutoa hitimisho. Hivyo basi, katika sehemu ifuatayo mtafiti amewasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni muhtasari, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya utafiti huu.

5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu umejikita katikakuchunguza vipengele vya Uhalisiajabu na namna vinavyoibua dhamira katika riwaya za Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kutaka kujua namna Mohamed Said Abdulla alivyotumia vipengele vya Uhalisiajabu na namna vipengele hivyo vinavyoibua dhamira katika riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili mahususi ambapo lengo la kwanza lilikuwa ni Kubainisha vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale ya* Mohamed Said Abdulla. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo ni vipengele gani vya Uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*?

Lengo mahususi la pili lilikuwa ni; Kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; Ni dhamira zipi

zinazobainishwa kutokana na matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale?*

Katika Utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imesaniiwa kwa vipengele mbaimbali vya Uhalisiajabu kama vile matumizi ya wahusika wa uhalisiajabu, mandhari za uhalisiajabu, uzungumzi nafsi wa kihalisiajabu, matukio ya kihalisiajabu, usimulizi wa kihalisiajabu, umahuluti wa kitamaduni, kitanzu na Mwingilianomatini. Ambavyo kwa ujumla ndivyo vilivyotumiwa na msanii kuibua dhamira alizozikusudia.

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi ya utafiti huu. Katika sura hii mtafiti amejikita katika kufafanua usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa utafiti huu.

Sura ya Pili inahusu mapitio ya maandiko ambayo msanii aliyatalii kabla na wakati wa kuandika tasnifu hii. Sura hii ina utangulizi na mapitio ya tafiti mbali mbali kuhusu riwaya na kazi zilizowahi kujadili uhalisiajabu. Sura hii pia imeeleza dhana ya dhamira na pengo la utafiti. Mwisho sura imewasilisha na kujadili nadharia zilizoongoza utafiti huu ambazo ni nadharia ya Uhalisiajabu na Mwitiko wa Msomaji na kumalizia hitimisho.

Katika Sura ya Tatu utafiti unaeleza mbinu zilizotumika kukusanya data hadi utafiti huu kukamilika. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni eneo la utafiti,

walengwa wa utafiti, sampuli na usampulishaji, kuaminika na kuthibitika kwa data za utafiti. Mwisho sura hii imemalizia kwa kutoa hitimisho.

Sura ya Nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Sura hii imeongozwa na maswali mawili ambayo yameigawanya sura hii katika sehemu mbili, ambapo sehemu ya kwanza imefanya uchambuzi wa vipengele vya uhalisiajabu vinavyojitokeza katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Uchambuzi wa sehemu hii ya kwanza umeongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu. Sehemu ya pili imewasiliswha na kufanya uchambuzi wa vipengele vya uhalisiajabu na namna vipengele hivyo vilivyoibua dhamira. Sehemu hii imeongozwa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Mwisho, sura hii imetoa hitimisho.

Katika Sura ya Tano tunapata hitimisho la tasnifu hii. Sura hii inabeba vipengele kama vile muhtasari wa tasnifu yote, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Ni katika sura hii ambapo matokeo ya utafiti huu yanaonekana na muhtasari wa tasnifu hii umewasilishwa kwa kubainishwa sura ya kwanza hadi ya tano.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu wenye mada inayosema Kuchunguza Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* baada ya mtafiti kukusanya data, kuzifanyia uchambuzi na kuziwasilisha kama ilivyobainishwa katika sura ya nne data hizo zimemuwezesha mtafiti kupata matokeo kama ifuatavyo:

5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni Kubainisha vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale ya Mohamed Said Abdulla. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni vipengele gani vya Uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*? Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imesaniiwa kwa vipengele mbaimbali vya Uhalisiajabu ambavyo ni matumizi ya wahusika wa uhalisiajabu, mandhari za uhalisiajabu, uzungumzi nafsi, matukio ya kihalisiajabu, usimulizi wa kihalisiajabu na umahuluti wa kitanzu, kiutamaduni na mwingiliano matini.

5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo mahususi la pili lilikuwa ni; Kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; Ni dhamira zipi zinazojidhihirisha kutokana na vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

Utafiti huu ulibaini kuwa, vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* vinaibua dhamira mbalimbali katika jamii zetu ambazo ni imani za jadi, uongozi mbaya, ukoloni, utabaka, mauaji, umuhimu wa kutunza kumbukumbu, upelelezi, uganga, unyonyaji na ukandamizaji na nafasi ya mwanamke. Hivyo msanii amebaini kwamba kila dhamira imewakilisha maisha halisi ya jamii nyingi za Kiafrika.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Katika utafiti huu mtafiti amebaini kuwa vipengele vya uhalisiajabu vimekuwa vikitumiwa na watunzi wa kazi za fasihi andishi ili kusawiri dhamira kadhaa za kijamii. Lengo la kutumia vipengele vya Uhalisiajabu ni kuibua dhamira na kuiakisi jamii kwa misingi ya ushabihi kweli. Kwa ujumla uhalisiajabu katika riwaya teule umetumika kama mbinu muhimu katika kufumbata dhamira za mtunzi.

5.4 Mapendekezo

Utafiti huu unahitimisha kuwa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imetumia vipengele vya uhalisiajabu ambavyo huibua dhamira. Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza mambo yafuatayo:

5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Utafiti huu ulijikita kuvichunguza vipengele vya uhalisiajabu na namna vinavyoibua dhamira. Hivyo ni wazi kwamba bado ipo nafasi ya kufanya tafiti nyengine katika kazi za mwandishi teule ama za waandishi wengine wa kazi za fasihi katika vipengele vyengine vya fani na maudhui. Kufanya hivyo kutapunguza pengo la kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili.

5.4.2 Mapendekezo kwa Watunga Sera

Utafiti unapendekeza kwamba ipo haja kwa watunga sera kuchukua mawazo yanayojadiliwa katika tafiti mbalimbali katika jamii ili kutatua matatizo kadhaa yanayoikabili jamii. Kwa kufanya hivyo tutaweza kujenga mustakabali mzuri wa

maisha ya jamii. Mathalani, katika utafiti huu ukoloni na athari zake umejadiliwa. Hivyo ipo haja ya kuweka mpango madhubuti ili kupambana na tatizo hili la kihistoria katika jamii za Afrika.

5.4.3 Mapendekezo kwa Taifa

Kwa upande wa Serikali inapaswa kuhamasisha wasomi juu ya swala zima la kufanya tafiti za kitaaluma ikiwemo katika uwanja wa fasihi ili kutunza tunu ya waandishi watangulizi ambao waliipa misingi imara fasihi ya Kiswahili tangu ndani ya Afrika hadi nje ya Afrika.

5.4.4 Mapendekezo kwa Jamii

Mtafiti anapendekeza kuwa wanajamii wawe na utamaduni wa kusoma kazi za fasihi ikiwemo zile za waandishi teule ili kutanua maaarifa na kuwawezesha kufanya matendo mema na kuepuka maovu yanayojadiliwa katika jamii na waandishi.

MAREJELEO

Abdalla (2015). Kosa la Bwana Msa na washauri wa Benki za Kiislamu. (www.likedin.com)

Abdalla na wenzake (2014). "*Utafiti na uandishi wa bibliografia dokezi ya Muhammed. S. Abdulla,"Kanzi ya Wanariwaya wa Kiswahili*. Morogoro: Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro.

Abdulla, M. S. (1982). *Mzimu wa Watu wa Kale.* Arusha: Eastern Africa Publishers Limited.Abrams, M. H. (1999).*A Glossary of Literary Terms*. Ithaca: Cornell University Press.

Alexander, M. (1990). *Flights from Realism.* London. Edward Anold.

Ali, H. A. (2015). Kutathmini Usawiri wa Mhusika Mwanamke katika Hadithi Simulizi zaWapemba.Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Allen, R. (2004). English Dictionary. England. Penguin Pogket:

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Cooper, B. (1998), *Magical Realism in West African Literature: Seeing with a Third Eye.* New York: Routledge.

Cresswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and MixedMethods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Danow, K. D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque.* Kentucky University of Kentucky Press.

Encarta Encyclopaedia (2002). New York. Microsoft Company Limited.

Enon, J.C. (1998). *Educational Research Statistics and Measument; Educational Psychology (2.ed),* Kampala: Makekere University Press.

Faki, A. M. (2015). Sifa za Utendi wa Kswahili Mfano: Utendi wa Fumo Liyongo. Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili (MA. Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Genette, G. (1972).*Figures Ill*,Paris: Seuil.

Green, M. J. A. (2009). Dreams of Freedom: Magical Realism and Visionary Materialism in Okri and Blake. Romanticism15/1: 18-32.

Hart, S. M. (2003). Magical Realism in the Americas: Politicalized Ghosts in One Hundred Years of Solitude, The House of S pirits and Beloved. *Journal of Iberian And Latin American Studies* 9/2: 115-123.

Herman, D. na wenzake. (2005). *Routledge Encyclopedia of Narrative Theory*. Abingdon: Routledge.

Homo, L. F. (2015). Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa Zao: Uhakiki wa Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo ya E. Kezilahabi.Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Mulika* Na 34 (uk 38-50)

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Ibrahim, W. N. (2016).“Uchambuzi wa Vipengele vya Uhalisiamazingaombwe katika Arusi ya Buldoza”.Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1983). “Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi” katika, *Makala za Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namba 3*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 226-243.

Khamis, S. A. M. (2005). *Arusi ya Buldoza naHadithi Nyengine*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Khamis, S.A.M. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novel.Research in African Literatures36/1: 92-108.

Khamis, Said A. M. 2007. The Swahili Novelist at the Crossroads: The Dilemma of Identity and Fecundity.*Swahili Forum* 14: 165-180.

Kinoti (2012). Nadharia ua Upokezi/ Mwitiko wa Msomaji. Kiswahili mambo leo. blogspot.com

Kisima cha Maarifa (2008). Uhakiki wa Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale. https//www.kisimachamaarifa.co.tz

Koenings, M.G.N.S.(2018). Mwana wa Yungi Hulewahttps://www.asymptotejournal.com/fiction/mohammed-said-abdulla-if-even-the-spirit-hild/swahili/

Kombo, D. K. na Tromp, D. L. A. (2006).*Proposal and Thesis Writing.* Nairobi: Pauline Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: WileyEasternLtd.

Kothari, C. R. (2008).*Research Methodology and Techniques*. India: New Age International.

Kothari, R. C. (2013). *Research Methodology: Methods and Techniques.* 2nd ed, New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Madumulla, J. S. (2011). *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historia na Misingi ya Uchunguzi*. Nairobi: Phoenix Publishers

Magaju, J. K. (2004).Kuchunguza Uhalisiajabu katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* na *Bin Adamu*.Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenya.

Mbatiah, M. (2001), *Kamusi ya Fasihi:* Nairobi Standard Text Books, Graphical and Publishing.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia,* Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishing

Mbatiah, M. (2002), *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi, Standard Textbooks

Mbia, G. O. (1961). *Three Suitors: One Husband*. Cameron:University of Keele.

Mhando, P. & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*.Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mkindi (2016), Maudhui katika kazi za fasihi.http://mwalimumkindi. blogspot. com/2016/08/maudhui-maudhui-ya-kazi-ya-fasihi.html

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mohamed, S. A. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Nairobi: Ramco Printing Works Ltd.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EALP.

Mturo, N, G. na wenzake (2018). Uhalisiamazingaombwe katika Muktadha wa Ubaada-Ukoloni: Mchango wa *Vita vya Mapenzi* ya Maundu Mwingizi: Mara Reaserch Journal of Kiswahili. Vol.3, No.1, June 2018, Page 22-31, ISSN 2520-0577, Nairobi: Idara ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi, M. M (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1983). Utafiti wa Fasihi Simulizi. Katika, Makala za Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Taaluma yaTaasisi za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mutiso, K. (2012). Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili. Katika *Mulika* Na. 31 uk. 115-133.

Mwakamele, I. (2013). “Introduction to Educational Research”.Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Misingi ya Nadharia za Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Nyambunga, V. A. (2005), ‘‘Uhakiki wa *Bina-Adamu*! (2002) na *Musa Leo* (2004) na Wamitila K.W, Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Omary, M. (2011). ”Siasa katika Ushairi wa Kazilahabi” Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Onchangu, R. Ny. (2013). Mtindo Katika Riwaya Na Hadithi Fupi Za Clara Momanyi. Nairobi: Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi

Olali, T. (2010). Structure and Anti-structure of a Swahili New Novel: A Stylistic Analysis of *Babu Alipofufuka*. The Nairobi Journal of Literature, UoN 82-98.

Osore, M. (2013). Magical Transformaions and the Subjugation of Nature in Said Ahmed Mohamed's *Babu Alipofufuka*. International Journal of Humanities and Social Science, 3(10), 132-136.

Panneerselvam, (2012) *Research Methodology*. New Delhi: PHI Learning Private Limited.

Prewitt, K. (1980). Introductory Research Methodology, East African Applications, Occasional Paper No. 10. Nairobi: Nairobi Institute of Development Studies, University of Nairobi.

Robnson, M. (1996). *Chambers 21st Century Dictionary. Great Britain: Cambrige University Press.*

Roh, F. (1925), *Nach- Expressionismus – Magischer Realismus, Probleme der neuesten europäischen Malerei*. Leipzig: Klinkhardt & Biermann.

Salim, M. A. (2015). Kuchunguza Ufasihi Simulizi Unaojitokeza ndani ya Hadithi na *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili; Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Saluhaya, M. A. na Suleiman, M. CH. (2012), *Nadharia na Tahahkiki ya Fasihi: Kidato cha Tano na cha Sita*. Dar es Salaam: STC Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.*Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2007). "Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe," katika *Kioo cha Lugha*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na fasihi, Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Singh, K. (2007). *Quantitative Social Reseach Methods*. New Delhi: SAGE Publication.

Waliaula, K. W. (2010), "Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*", Swahili Forum 17:143-157.

Wamitila (2008).*Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Vide Muwa Publishres Ltd.

Wamitila, K. W. (2002).*Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*.Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo's *Pedro Paramo*. Kiswahili66: 49-58.

Wamitila, K. W. (2004). *Musaleo!* Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. W. (2008).*Kanzi za Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2013), “Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili”, katika *Mulika* namba *32*.TATAKI*:* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Wanjiru, M. J. (2013). Uhalisia Na Uhalisiajabu Katika Riwaya Mpya: *Babu Alipofufuka* (Said Ahmed Mohamed) na *Watu Wa Gehenna* (Tom Olali).Tasnifu yaShahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Warnes, (2006).*Magical Realism and German Idealism.Modern Language Review* 101/2: 488-498.

Yin, R. K. (1994).*Case Study Research: Design and Methods*. Oaks Calif: SAGE Publishers.

Zamora, P. L. na Faris, B.W. (1995). *Magical Realism Theory:* History Community, London: Duke University Press.